ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Saba - Tarehe 24 Juni, 2016

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni ya 63, inasema "Mjumbe anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu".
Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa, kwa huzuni kubwa, kwa unyenyekevu mkubwa, naomba msaada wa kiti chako. Wewe shahidi na Mwenyezi Mungu anajua, mara nne au mara tatu ninasimama kwa hoja hii.

Mhe. Spika: Samahani Mheshimiwa anza tena sijakufahamu unaomba, hilo ombi lako nilikuwa naomba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nikushukuru sana kabisa kuniruhusu kusimama hapa. Kwa masikitiko makubwa, kwa huzuni kubwa, kwa huruma kubwa, kuna jambo limetokea jana utafikiri tuko Burundi nimemuonea huruma sana Mheshimiwa bosi wangu Ali Suleiman Shihata kwa kadhia iliyomkuta jana kwenye jimbo lake, alihangaika muda mrefu na tumesema muda mrefu suala hili, serikali itoe kauli. Jana utafikiri tuko Burundi Mheshimiwa risasi zilivyolia.

Nataka muongozo wa kiti chako kuhusu kauli ya serikali kwa suala hili. Muda mrefu tunaambiwa litakuja suala hili na keshokutwa tunafunga Baraza. Jana tumelizungumza matokeo yake kuna watu watatu wamepigwa risasi wako Al-Rahma, nafikiri wengine wakapelekwa Mnazi Mmoja, kitendo kilichotokea jana. Kwa hivyo Mheshimiwa nataka muongozo wa kiti chako siku zinakwenda au kama nilete hoja ya dharura ile utaniruhusu Jumatatu niwasilishe. Nataka muongozo wako, hali hairidhishi utafikiri tuko Burundi Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nitatoa muongozo baadae kwa kuruhusu labda serikali kama watakuwa na lolote ambalo wataweza kulizungumza halafu wataweza kukujulisheni. Tunaendelea.

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: *Bismillahi Rahmaani Rahiim.* Namshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kunipa uzima na nakupongeza sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kwanza bila kusahau kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha kwa kazi yake nzuri pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri waliyoanza nayo. Vile vile nitazungumzia machache ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha kwa kumshauri pamoja na kuzungumza yale ambayo yaliyofanyika nyuma.

Mimi Mhe. Spika, nitazungumzia kwanza nitataka kumwambia Mhe. Waziri wa Fedha yeye ndiye waziri ambaye atakayeweza kusimamia matumizi mazuri ya Serikali yetu ya Zanzibar na wizara yake pindipo itatetereka basi uchumi wa Zanzibar umetereka vile vile. Nitamuomba sana wizara yake ahakikishe kwamba inasimamia vizuri, ina-*collect* pesa vizuri, ili mambo yaende vizuri ndani ya serikali yetu. Lakini mimi leo nitazungumzia mambo 3. Nitazungumzia mradi wa barabara ya Kwerekwe/Fuoni, nitazungumzia mradi wa *Terminal II Airport*, nitazungumzia mradi wa AGAPE na mambo mengine.

Mhe. Spika, mimi ningeanza na mradi wa *Terminal II Airport.* Mhe. Waziri wa Fedha *Terminal II Airport project* yake ilianza mwaka 2009, na hii *Terminal II* ilikuwa imeanza na *projec*t ya dola milioni 7.4 kwa kuanza 2009. Baadaye mbele ikapanda dola milioni kumi na moja laki nane na ishirini na nane mia sita na sabiini nne ikapandishwa tena. Baada ya hapo *airport* hii hii ikapandishwa tena dola milioni arubaini na sita, laki tano na elfu kumi na nane mia nne na kumi na nne. Na hatimaye mpaka sasa hivi *airport* hii imetimia dola milioni 128,747.89.

Mhe. Spika, naomba sana kumuambia Mhe.Waziri wa Fedha mradi huu naweza kusema kwamba mradi huu sio halali, kwa sababu inaonekana dhahiri kuna mambo machafu yamefanyika sana kwa mujibu wa bei hii ya *airport* iliyojengwa *Zanzibar Terminal II* udogo wake na bei iliyojengwa basi itakuwa *the most expensive small airport in the world.* Ni *airport* ambayo ukimleta mtu yeyote, *engineer* yeyote, kampuni yoyote basi haiingii akilini pesa hii iliyotumika katika *airport* hii. Huu ndio ukweli na hii inaonesha dhahiri kwamba hapo nyuma ninamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha awe makini

sana, la sio hivyo atakuja kuingizwa katika kitu ambacho hakimuhusu na mimi ninampongeza sana hili jambo yeye kaingia ndio kwanza kaanza nalo. Lakini hili suala ni kubwa, hizi ni pesa za wananchi waliokuwa maskini zimetumika vibaya.

Jambo hili linasikitisha zaidi kwamba mkopo huu nafikiri serikali italipa mkopo huu mpaka vijukuu tutaukuta mkopo huu. Kwa sababu ni fedha nyingi sana ambazo sio za kweli. Mimi ninamhakikishia sana pia na Mhe. Rais ninamhakikishia kwa ujenzi wa *airport* hizi fedha sio kweli zilizotumika haiwezekani. Ile *airport* kwa mujibu ilivyo *airport* yenyewe hata kiwango haina, ilivyopangwa mpaka hivi sasa kunatuama maji kwenye *airport* pale mbele. Ndege kubwa ziki-*park* zinagusa ile *airport*.

Mhe. Spika, cha ajabu zaidi kwamba viongozi waliopita baadhi yao walimchukua Mhe. Rais kwenye *airport* ile na kumuahidi kwamba *airport* ile watamkabidhi kabla ya sherehe ya Mapinduzi wakatoa ahadi leo wanafanya mambo ya kipuuzi ambayo wanamfanya mpaka Mhe. Rais anaonekana labda anazungumza vitu ambavyo havipo.

Mimi naomba sana watu hawa wote waliofanya mambo haya wachukuliwe hatua, na naomba sana Mhe. Spika, kwa kupitia Waziri wa Fedha tuunde Kamati, bila ya malipo tuko tayari kwa ajili ya kuchunguza suala la *airport*. Hatutaki malipo shilingi hata ya mafuta hatutaki, tuko tayari kuunda kamati kuchunguza hili suala, pesa za wanancni wanyonge waliodhulumika. Hata hawa ambao wanaturuhusu sisi kupata mkopo mwisho watachoka, *Exim Bank* iliyotupa mkopo ulifikiri hawajui hivi vitu bei zake, hii Mhe. Spika, hata tukileta *contractor* wa Ujerumani ile *airport Terminal II*, hata 45 *million dollars* haifiki. Leo tunaambiwa dola milioni 28 zimeshatumika mpaka sasa hivi wakati *airport* ile pale hata kumaliza haijamaliza. Cha ajabu zaidi kwamba ile *airport* hata *VIP* ndani hakuna, *cargo area* hakuna, *airport* haina kiwango.

Mimi ningeomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha tunataka tuunde Kamati ya kuchunguza suala la *airport*. Dola milioni 128 haiwezekani dunia nzima ujenzi huu hauwezekani, ukiifanya *airport* ile hata kwa *square metre* moja basi hata hiyo *pentagon* na majumba ya Dubai lile *tallest building in the world* haijafikia kwa *square metre* moja. Tusidanganyane, mimi ninamuomba sana Mhe. Rais kwa hili hapa ikiwezekana hata *airport* kwa sasa hivi isubiriwe, isiendelezwe mpaka tutafute kamati ichunguze, na sisi tupo tayari wala hatutaki malipo kwa ajili ya kuchunguza pesa za wananchi, pamoja na pesa hizi zirudi kwenye serikali.

Kampuni yoyote inayojenga ma-*airport* au mabandari lazima inakuwa na *full insurance*, na kama tutakuja kukukamata hii suala basi kampuni ile itabidi irejeshe pesa serikalini na wale ambao waliohusika wote waje washtakiwe, haiwezekani kabisa *airport* hii ikatumie dola milioni 128. Mimi binafsi niko tayari kushirikiana na serikali kuleta kampuni yoyote ya *European countries* tuje tufanye utafiti muone kama itafika dola milioni 60 *airport* ile.

Mhe. Spika, inasikitisha sana, kuna mambo yanaonekana dhahiri tunamuangusha Mhe. Rais, anatuamini lakini utendaji unakuwa mbovu, tunaiangusha serikali, tunakiangusha chama, tunawadhulumu wananchi waliokuwa maisha yao ya chini. Fedha ni nyingi sana zinaonekana dhahiri, mimi nasema moja kwa moja huu ni wizi uliofanyika hapa, dola milioni 128 haiwezekani kwenye *airport* hii. *Airport* hii kwa mujibu ilivyo hata dola milioni 60 haifiki, leo fedha hizi tunaambiwa fedha ya madeksi hakuna, madawa hakuna, matokeo yake watu wanaiba kwa njia nyengine, hii ni dhahiri kabisa, ni wizi umefanyika hapo nyuma.

Ninamuomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha tuunde Kamati kwa hili tena bure hatutaki shilingi ya mtu tulipwe, tutafanya kazi kwa ajili ya wananchi na kwa ajili ya serikali ili serikali isipate hasara.

Vile vile mimi nitakwenda kwenye mradi mwengine mradi wa AGAPE. Mhe. Spika, huu mradi umeshatumia *almost 10 billion shillings*, serikali ishalipa lakini mpaka sasa hivi hakuna kilichofanyika wala hatukioni. Mpaka sasa hivi ukiangalia huu mradi unasema kwamba kuna *shares* 30% zinakwenda kwenye *ZBC*, 40% zinaonekana kwenye Wizara ya Fedha na 30% zinakwenda kwenye Wizara ya Habari. Lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika kinachoonekana, ukiangalia vile vile TV mpaka leo inamwesa mwesa, kila kitu kiko taabani, hizi fedha zimefanyika nini, mimi nitataka kuja kujua.

Vile vile kila kitu kinapofanyika kuna *feasibility study* inafanyika, hivi kweli wale, naruka kidogo naingia tena kwenye *airport* wale ma-*engineer* waliotumika au viongozi waliotumika kwenye lile suala ni wendawazimu. Leo *airport* imeshajengwa wanakuja kuambiwa haitimii, inajaa maji ndege zikiegeshwa zinagonga, hao ma-*engineer* walikuwepo wapi? Michoro ya mwanzo ilikuwa inasema vipi? Inaonekana dhahiri kwamba kumepita kitu cha udanganyifu, na mimi kama Mwakilishi wa Chaani hili suala sikubaliani nalo na nawaomba wenzangu tuungane tuunde kamati, na Mhe. Rais tunamuomba pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu mradi wowote wa fedha kama hizi na yeye unamuhusu ili tufuatilie. Hatutaki malipo, nasema tena malipo hatutaki kwa suala hili.

Mhe. Spika, narudi tena kwenye AGAPE pesa nyingi sana zimeshatumika leo tunaambiwa zinataka kuja kutumika nyengine, hivi vitu mbona vinakwenda kitendawili, hivi vitu mbona kila siku havimaliziki. Mimi nashangaa kila siku kwenye *project* za serikali maisha yote zinakuwa zina mazishi ndani hazimalizi, hata zikimaliza utakuja kuambiwa mwisho kuna kitu kimefeli.

Nitatoa mradi mdogo tu mradi wa Pemba Ofisi ya Wizara ya Fedha imejengwa, matokeo yake sasa hivi inatuama maji haitumiki, ni vitu ambavyo *non sense*, haviingii akilini, ma-*engineer* walikuwepo wapi, watu wa ukaguzi wa mambo ya *drainage* walikuwepo wapi, ni hayo yaliyotokea *airport*.

Mheshimiwa kuna ubadhirifu mkubwa na safari hii Baraza hili ndio litaanzaa kutumbua majipu kumsaidia Mhe. Rais, tupo tayari kufanya kazi hii. Mimi ninachosema Mhe. Spika, Mhe.Waziri wa Fedha hatumuogopi mtu, na wote wanaohusika kwenye suala hili tutaisaidia serikali, tumsaidie Waziri wa Fedha, tutakusaidia Mhe. Spika, kwenye hili suala kuliweka sawa. Haogopewi mtu hapa, kwenye suala la kweli litazungumzwa kweli, kwenye la haki litazungumzwa haki, na kama mtu kaiba tutasema kaiba na kama kuna mtu kadanganya tutasema kadanganya.

Mhe. Spika, mimi nakwenda kwenye suala la mradi wa barabara ya Kwerekwe mpaka Fuoni. Ule mradi unasemekana kwamba *plan* ya mwanzo ilikuwa kumpa *MECCO* kwamba atie kifusi lakini lami itakuja kutia serikali. Lakini ninachomuomba Waziri wa Fedha ile barabara ni muhimu sana, leo watoto kule wanachezea mavumbi wanaosoma watoto wadogo, itasababisha matatizo ya kifua, mambo ya *cancer*, mambo ya maradhi ya macho kwa sababu tu ya mavumbi, njia muhimu njia kubwa, ina matatizo makubwa, ina uchafu mkubwa. Keshokutwa tutakuja kuambiwa imeharibika kifusi, maana yake kifusi chenyewe tunachokijua cha ujanja ujanja sio kifusi ya uhakika. Itakuja kuambiwa kishaharibika serikali igharamike tena au tutangojea mpaka serikali iingie gharama tutumie tena.

Mimi ninamuomba sana Mhe. Waziri suala hili alisimamie, na ninamuomba sana Mhe. Waziri kwa wadhifa alionao aangalie sana katika mambo yake yote ya *project* zote zinazokuja, miradi yote aichunguze vizuri au asimamie mwenyewe, la si hivyo atakuja na yeye mwenyewe kuuzwa.

Watu wajanja, watu wizi, mimi Mhe.Waziri ninamuamini sana, muaminifu lakini akifanya mas-hara na yeye mwenyewe atauzwa bila kujijua. Siku hizi mtihani, leo gari ya mtu ya dola laki moja atakwambia dola laki mbili, mimi

nitamwambia Mhe. Waziri achunguze mwenyewe au ikiwezekana akanunue mwenyewe gari Dubai.

Natoa mfano mwengine fedha hii inayolipwa hapa ndani ya Zanzibar kujenga barabara kilomita moja basi ni tani 20, mfano tani 25 *wallahi laadhim European Standard* kwa bei ile ile unajenga kwa tani 60, na wako tayari kuja kujenga. Haya mambo ya ajabu, msifanye watu hawana akili, watu wanaona, tusidhulumu watu. Leo Serikali inasema haina fedha kumbe kuna wajanja wanaiba, tutakaa tuwaachilie mpaka lini, safari hii mimi nasema watakoma kwenye Baraza hili. *(Makofi).*

Yoyote yule tutakayemkamata, tutakayejua hatutomficha, hatutoogopa mtu. Mhe. Waziri wa Fedha ninakuomba sana kwa kushirikiana na Waziri wa Mawasiliano simlaumu yeye wala sikulaumu wewe, nyote wapya kwenye wizara hii, lakini wale wote wanaosababisha matatizo haya kutia serikali hasara, kutia wananchi hasara na kumuadhirisha Mhe. Rais kwa ahadi za uongo hawa wote wachukuliwe hatua. Kila siku Mhe. Rais mnamchukua mnampeleka huku mnampiga *date* za uongo, maneno ya uongo, mumeaminiwa jiaminisheni! *(Makofi).*

Leo wananchi wote wanaona Mhe. Rais saa nyengine anadanganywa na yeye hawezi kufanya kazi zote, yeye Rais ana viongozi wake, jiaminisheni msimdanganye, mnamtia aibu, mnatia aibu chama, mnatia aibu serikali, mnamtia Mhe. Rais aibu, haipendezi.

Mhe. Spika, ninakuhakikishia kamati utakayoiunda ukitukubalia na Mhe. Waziri wa Fedha tutafanya kazi kihalali, na utakuja kuona hapa tutamtaja mmoja mmoja aliyehusika na suala hili. Na ninakuhakikishia tena *airport Terminal II* dola milioni 60 haifiki mpaka inamaliza. Na niko tayari mimi nipewe na wenzangu tuishughulikie tutajenga kuliko ile kwa dola milioni 60. Haya ni masuala ambayo tunataka tupunguze ujambazi Zanzibar, Zanzibar kuna ujambazi wa hali ya juu kwa wananchi wa chini.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha mimi ushauri wangu ndio huo, wizara yako ni ngumu, mambo mengi yanayohusu mradi mkubwa, mdogo, nakuomba sana simamia mwenyewe na viongozi mnaowaamini mkatenda haki kwa wananchi kwenye mfuko wa serikali, ili serikali ika-*save* pesa zisije zikaenda kwenye matapeli.

Mambo yote nakuomba sana miradi yote sasa hivi hakikisha kwamba unaisimamia na unaijua. Leo *contractor* unaambiwa kilomita moja 1 *billion*

shilling, twenty tons of road wakati hiyo 1 *billion shilling* dola laki tano unajenga tani 60 ya barabara na ina *garantee* ya miaka 25. Leo barabara Zanzibar zinajengwa miaka 2 zimeshaanza kufanya matuta na mashimo tunasapotiana, tunasapotiana nini na tunafanya mambo ya uongo.

Mhe. Spika, vile vile mimi naomba sana tuunde kamati, ninamuomba Mhe. Waziri wa Fedha atukubalie, kamati bila ya malipo, ninamuomba Mhe. Rais, hatutaki mafuta, hatutaki posho, tukachunguze suala la *airport*, tukachunguze AGAPE, tukachunguze na mambo mengine, tuko tayari kufanya kwa ajili ya wananchi, hatujaja hapa kukaa kupokea *sitting allowance* na mishahara, sisi sote Wawakilishi tumekuja hapa kufanya kazi hatutaki fedha sisi.

Hapa tunataka tupate mshahara tupate *sitting allowance* hapa tunataka tupate mshahara *sitting allowance* kwa halali, tunafanya kazi hatujaja kukaa tu bure bure, hii ndio kazi yetu.

Mimi ninamuomba sana Mhe. Rais kama hajasikia naomba taarifa ipelekwe, lakini tunataka kamati bila ya malipo na tutamfanyia kazi na fedha zitarudi. Na ile kampuni kama imeshiriki kudanganya na baadhi yake wengine basi fedha zitarudi na tutazishtaki.

Mimi nitaishia hapo ninampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na watendaji wake kwa uzoefu wao mzuri, kwa uaminifu wao, lakini nimezungumzia nyuma yaliyofanyika awe *careful* sana, la si hivyo narudia tena atakuja kutiwa kwenye jina baya wakati yeye hahusiki na mambo hayo. Namuomba sana Mhe. Waziri awe makini, vitu vyote avifuatilie. Mimi ninaisapoti bajeti hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuweza kuendelea mwezi wetu mtukufu wa Ramadhani. Lakini nichukuwe nafasi hii tushukuriane sote katika hili na pamoja niipongeze bajeti iliyosomwa na Mhe. Waziri wa Fedha kaka yangu Dkt. Khalid pamoja na Mwenyekiti, kwa kazi nzuri wanayoifanya na yenye hekima, busara na usikivu mkubwa.

Mhe. Spika, wizara hii nathubutu kusema ina watalaamu wazuri *Alhamdulillah*, niipongeze Wizara ya Fedha, niwapongeze watendaji wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Makamishna wa *ZRB*, *TRA*, *Income Tax* na sehemu zote zile ambazo nilizokuwa sijazitaja.

Kwa kweli Mhe. Spika, wizara hii ni wizara ambayo inaweza kutuletea neema kubwa sana, kutokana na watendaji wake kuwa na uwezo wa kukusanya kodi na kupata nguvu za sisi kutekeleza ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii vile vile kutoa wito kwa wafanyabiashara sote, nikiwemo na mimi Raza, basi tubadilikeni, angalau kuweza kulipa kodi ili humu ndani tunapokaa tuweze kutekeleza ilani ya chama kwa kuwaletea wananchi maisha bora kama maji, umeme, kilimo na mambo mengine, makusanyo haya ndio yanayokwenda kwa wananchi. Kwa hivyo, niombe tu kwamba hakuna mfanyabiashara anayekula hasara, lakini na sisi tunatakiwa vile vile tubadilike katika kuiunga mkono Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri Dkt. Khalid, nimuombe sana kwa bahati nzuri amekulia Donge, sasa mimi nimuombe tu kaka yangu Dkt. Khalid haya maneno yanayozungumzwa ya *AGAPE* na ya *Airport* yana uzima. Kwa hiyo, nimuombe tu Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wasilichukue hili jambo la kawaida, suala hili la kigugumizi, la *AGAPE* ambayo serikali imeshatumia *over 8 billions* hapa Mhe. Nadir alisema pamoja na Mradi wa *Airport* ambayo ishatumika *128 million dollars*.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri sehemu zote mbili hizi mimi nilikuwa Mjumbe na hii ya mawasiliano Mwenyekiti wangu msikivu, Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye tunakwenda nayo. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri haya mambo yana ukweli, suala hili la kigugumizi la *AGAPE* nilisema lakini tatizo letu Mhe. Spika tunapozungumza kwa wizara zinazohusika hawaji na majibu, hawaji na majibu kabisa.

Kwa hiyo, suala hili la kigugumizi la *AGAPE* tulikuwa tunalizungumza leo karibu miaka miwili Mhe. Spika. Mhe. Spika, hapa hamna kitu ndani ni sawa sawa na kulibeba pakacha ukaweka maji. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwa hili awe msikivu kwa Wawakilishi, kwa sababu wizara yake sio inayohusika lakini yeye ndiye mtoaji pesa anazosimamia. Mradi wa *AGAPE* ni wa vigugumizi, hakuna chochote Mhe. Spika, ni mradi ambao umeumiza Taifa letu la Zanzibar, Makatibu Wakuu hawakushirikishwa katika mradi huu, ulipelekwa tu kwenye Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, mimi nina ushahidi wote kwa sababu nilikuwa Mjumbe mle, hata hiyo *ZBC* Mkurugenzi ambaye alitakiwa hawakushirikishwa. Halafu leo tunakwenda kuongeza pesa, mradi huu ulikuwa wa dola 3,000,000 ushahidi wote upo. Kwa hiyo, nimuombe tu Mhe. Waziri na watendaji wake, Katibu

Mkuu Ndugu Khamis Mussa wasibebe kifua kwa jambo hili kwa Mwenyezi Mungu walifanyie kazi, wenzangu kama kuna kamati lifanyiwe kazi tupate vitu vya uhakika.

Mheshimiwa hapa tumekuja kutekeleza ilani ya chama, hivi sasa sote tunagombana humu ndani, mimi barabara hamna, dawa hamna, maji hakuna, umeme hakuna, lakini serikali yetu si mpaka ipate ndio itumie. Kwa hivyo, niombe tu Mhe. Spika mradi huu na Mradi wa *Airport* kwa kweli mimi naweza kusema ni shaghala baghala tu maana yake. Lakini kuna utaratibu, kwa hiyo nimuombe Mhe. Waziri kwamba huu ushahidi upo, mimi nilishiriki, akitaka anite mpaka sehemu za huo mradi kigugumizi Mheshimiwa, hata hii *ZBC* inavyoruka si matatizo ya awali ni matatizo ya kigugumizi, hakuna tija, hakuna tulichokipata.

Mhe. Spika, nilitoa hoja yangu mimi kwa waziri anayehusika Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo lakini mheshimiwa tunakuja mtu anauliza swali hata kujibiwa hajibiwi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha alipokee, naamini Wawakilishi wote watakuja, kuna ukweli wa hili mimi nina ushahidi kwani nilikuwa mjumbe katika wizara ile iliyopita. Kwa hivyo, ninaijua *in and out,* wala mtu hawezi kunidanganya kwani nilikuwa mjumbe na ninazo nyaraka.

Pia na hii Kamati ya Mawasiliano mimi mjumbe pia ninazo nyaraka. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri na watendaji wake kina Khamis Mussa wasije wakafika pahala kwa sababu wanaheshimika sana, wizara hii mheshimiwa ni wizara ya kihistoria katika nchi yetu ya Zanzibar lakini nataka wawe wasikivu.

Pia niwaombe mawaziri kaka zangu mimi ni mdogo wao kwa hili, bora tulitafutie mapema *solution* ya kusema tunapata kamati au serikali inaandaa taratibu ya kuleta hoja binafsi. Lakini kwa kusema kupiga buti tutakwenda kwenye dhambi na sote tumefunga Mheshimiwa haya mambo yana ukweli, pesa zimetumika. *Exim Bank* wameanza hiyo kwa makusudi, wao biashara, tutakwenda wajukuu zetu na vilembwe. Kwa hiyo, mheshimiwa nimalizie hapo ya kwanza.

Mhe. Spika, jambo la pili nije katika ukurasa wa 26, Benki ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi niipongeze benki hii, niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, leo imethibitisha kwamba benki hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni mmiliki pekee wa *PBZ*. Nakushukuru sana Mhe. Waziri, unajua

mheshimiwa *PBZ* sasa hivi ilipo, wao kila mtendaji pale *it's a private* ni kama shamba la bibi, *I have evidence*.

Mhe. Spika, sisi tuipongeze *KCB* leo hapa, tuipongeze *Exim Bank*, benki zote tuzipongeze kama tungelikosa benki hizi leo *PBZ* tungeliumia sana. Mhe. Spika, *PBZ* haipo, kwa baadhi ya watendaji haipo.

Kuna pesa zinatiliwa kwa wafanyabiashara mabilioni tena wanatiliwa bure, ushahidi upo Mhe. Spika. Baadhi ya Wajumbe wa Bodi na baadhi ya watendaji, baadhi nasema, sio kila anayepepesuka ni mlevi.

Mhe. Spika, *PBZ* tutafika wakati tutawaambia wafanyabiashara huko siko, lakini bado tuna imani kwa utendaji na serikali imetamka wazi hapa. Kwa hivyo, serikali ichukue hatua ya kuweza kulifanyia kazi suala la benki hii.

Mhe. Spika, benki hii leo kuna baadhi ya Wajumbe wa Bodi *regulator* Benki Kuu wametoa taarifa serikalini kwamba huyu mtu hafai. Lakini hapa leo tunasema huyu nimecheza naye mpira, huyu sijui nimesoma naye darasa moja, huyu sijui rafiki yangu, mpe laki tano kwa mwezi atumie kama rafiki yako, lakini asiharibu nchi. Kama rafiki yako, ndugu yako, umesoma naye skuli moja basi mpe posho katika mshahara wako. Kwa hivyo, Mhe. Spika *PBZ* baadhi ya watendaji kuna ushahidi wa kutosha mabilioni ya pesa wameingiziwa wafanyabiashara halafu anaendewa mfanyabiashara anaambiwa aah basi toa kidogo tu *ten percent*.

Mhe. Spika, ushahidi upo bilioni wametiliwa baadhi ya wafanyabiashara na wengine walikuwa wazalendo wanaipenda nchi yao. Kuna mfanyabiashara mmoja ametiliwa zaidi ya bilioni amerejea serikalini pesa zile zirejeshwe, hii *PBZ* na wajumbe wao wa bodi, ushahidi upo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuna mfanyabiashara ametiliwa mabilioni ya pesa nje tena dola zaidi ya dola nusu milioni *cash* ametiliwa. Lakini mfanyabiashara yule kwa sababu anapenda nchi yake, ana uchungu na nchi yake basi pesa zile alizirejesha lakini alishaambiwa kwamba basi tugawane. Sasa baadhi ya Wajumbe wa Bodi wamekuwa siku hizi kama ni wateja kwa watu mitaani, maana kuna baadhi ya Wajumbe wa Bodi Mhe. Spika kutwa wako mabenki. Kwa hiyo, wewe ni Mjumbe wa Bodi imekuhusu nini benki siku zote.

Kwa hiyo, kuna baadhi ya Wajumbe wa Bodi, nasema baadhi, sio kila anayepepesuka ni mlevi, kama serikali haikuchukua hatua Mhe. Waziri wa Fedha na huu mkopo ni kiini macho tu, watwambie wametoa bilioni hamsini

wanasema. Huu mkopo huu mheshimiwa mtu ameweka nyumba ya milioni mia amepewa mkopo wa milioni mia nane, huu ndio ukweli na ushahidi upo.

Mhe. Spika, unajua *funika kombe mwanaharamu apite*, lakini kuna vitu vingi. Leo mtu anapeleka kwa sababu Mjumbe wa Bodi jamaa yake wanafanya biashara pamoja anapeleka nyumba ya milioni mia, anataka mkopo wa bilioni. Lakini Mheshimiwa katika mazingira haya ninaiambia serikali, ninaiambia Wizara ya Fedha kwa sababu tuna ushahidi wa kutosha, kama serikali haikufanya ukarabati wa baadhi ya watendaji yaani mheshimiwa pale kutwa *management* tena ukienda wanakwenda kujipangia biriani mchana, ni kithiri biriani hasa mchana eti wanakaa kikao.

Halafu Mhe. Waziri wa Fedha nikuombe hii kama benki ya serikali hakuna haja ya kukodi ndege nzima watu wakafanya kikao Pemba, kwa kitu gani? Mnakodi ndege nzima watu wanakwenda kule kikao cha bodi Pemba, kwani nyumba yako ile.

Mhe. Spika, pesa hizi ni za wananchi Mzee Abeid Amani Karume Marehemu aliitengeneza benki hii kwa maslahi ya wananchi bila ya kujali rangi, kabila wala dini. Mhe. Spika, hilo nimeona nilizungumze na kuna *evidence* kwamba tusipoona hilo basi benki itakwenda zake, na baadhi ya watendaji tena wakubwa wamekuwa tena pesa hizo zinakwenda tu, ndio maana tukakuta sasa hali hii tuliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, nije katika *BoT*. Mhe. Spika, juzi tulikuwa na sherehe ya kutimiza miaka 50 ya Benki Kuu. Nilitaka nijue tu Mhe. Waziri wa Fedha atupe taarifa. Benki Kuu juzi wamekamilisha miaka 50, na Benki Kuu ni benki ya Muungano kati ya Zanzibar na Tanganyika ndio ikaitwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, lakini Mheshimiwa juzi tulipoona tulimuona Rais wa Tanzania Bara, hatukumuona Rais wa Zanzibar, hatukumuona Waziri wa Fedha lakini kule tulikuta watu wanasheherekea miaka 50 ma-*Gavana* wote walialikwa; wa Zambia, Uganda, Zimbambwe, Kenya, South Africa. Lakini hatukumuona Rais wa Zanzibar maana yake lile ni suala la uhai wa nchi, Benki Kuu bila ya Zanzibar huwezi kuita *Bank of Tanzania.*

Kwa hiyo, sasa nataka Waziri wa Fedha atwambie Rais alikuwa na dharura, kama alikuwa na dharura ni sawa, na je, Waziri wa Fedha alikuwa na dharura aje atwambie. Lakini isifike watu pale akakaa *Gavana*.

Mhe. Spika, juu ya hivyo Benki Kuu hii juzi walisema wamechangia madeski mabilioni. Nataka nimuulize Waziri wa Fedha aje kutwambia Zanzibar katika

mchango huu wa Benki Kuu ni kiasi gani tumetengewa Zanzibar, na Wizara ya Fedha inashiriki vipi katika utaratibu huo.

Mhe. Spika, nikimalizia hapa Benki Kuu tulikuwa na utaratibu wa kuweka makusanyo, sasa makusanyo haya na 1994 tukawa hatujamaliza, 1996 kuhusu *shares* zetu katika Benki Kuu na utaratibu. Nataka Mhe. Waziri atupe *updates* Mhe. Gavana Mkuu Benno Ndulu wakati katika miaka mitatu ya Bunge la Katiba la Dodoma alisema kwamba Zanzibar haikuchangia. Sasa nataka Waziri wa Fedha aje atwambie hapa anasema Gavana Mkuu Dodoma kwamba Zanzibar haikuchangia hata shilingi tano katika Benki Kuu. Yeye yule ni muajiriwa Mhe. Spika, kwanza nataka Mhe. Waziri atwambie halafu atuombe radhi, yule ni muajiriwa tu kaajiriwa. Kwa hiyo, kama ni *professor* alikuwa akutane na serikali mbili, akutane na Marais wawili lakini alithubutu kusema kwamba Zanzibar haikuchangia Benki Kuu ya Tanzania, *document* ipo na kaseti ipo Waziri wa Fedha aje atwambie hapa…

Mhe. Spika: Una dakika moja Mheshimiwa.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Spika, nizungumze suala la mwisho la *OIC*.

Mhe. Spika, Mzee wetu Magufuli amekuja na biashara ya viwanda na sisi tunataka sasa hivi tubadilike, suala la *OIC* ni suala la shida. Kwa hiyo, ningeliiomba serikali sasa katika kutafuta miradi ya uchumi hili suala la *OIC* lisiwe la mjadala, tuweze kujiunga na *OIC* ili Wazanzibari wapate maendeleo.

Mhe. Spika, suala la *OIC* yalikuwa ni makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania Bara na Serikali ya Zanzibar kwamba Zanzibar ijitoe kwenye *OIC* tuingie Tanzania na ushahidi upo. Dkt. Salmin Amour Juma alitwambia pale Rais Mstaafu kwamba Zanzibar imejitoa ili Tanzania ijiunge tunufaike sote. Kwa hivyo, kama ndugu zetu Bara hawakuwa tayari watuachie sisi Zanzibar inakuwa ni shida, wao kama hawataki sisi hawakubali, wao wakitaka sisi tukubali. Hivyo haiwezekani Muungano wetu huu ni wa sawa mheshimiwa, wakati wa Mwalimu Nyerere tulikuwa na *passport* inaandikwa usiende Israil. Leo Serikali ya Tanzania Bara inazungumza kufungua ubalozi wa Israil na wakati Mwalimu Nyerere ndani ya *passport* ilikuwa inaandikwa huwezi kuhudhuria.

Kwa hiyo, tubadilikeni, tunaitaka sasa *OIC* na taasisi zote za kuweza kutusaidia. Kauli hii aliitoa Kamandoo labda muniambie hapa Komandoo na yeye siye, maana kila mtu ndiye, siye. Sasa tuambieni Dkt. Salmin Amour

Juma alitoa kauli na mikataba ya makubaliano ipo kwamba Zanzibar ijitoe Tanzania ijiunge tunufaike sote, Tanzania haikufaidika.

Mhe. Spika, naunga mkono Wizara nzima ya Fedha kupitia Dkt. Khalid kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini nakubali yote hayo kutokana na watendaji wake.

Mhe. Spika, narudia kusema kwamba nakushukuruni, naunga mkono zaidi ya asilimia mia kwa Wizara hii ya Fedha. Lakini Mhe. Waziri wa Fedha nakuomba na watendaji wako muwe wasikivu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kupata nafasi hii muda ambao ni mapema sana katika kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* asubuhi akatujaalia bado tukawa ni wazima wa afya na tukaendelea na majukumu yetu kwa mujibu wa kanuni, katiba na sheria ambazo tunazo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo napenda nichukue fursa hii kuendelea kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Micheweni kwa kuendelea kuniamini.

Vile vile napenda nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza sana Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa muelekeo mpya wa jinsi gani ambavyo katika kipindi hiki tutaendelea kwenye mwelekeo mzima wa ukusanyaji wa mapato ya serikali hii.

Mhe. Spika, moja kwa moja naomba nianze tu kwa kuchangia kwenye masuala mazima ya ukusanyaji wa kodi.

Mhe. Spika, mimi kwa uoni wangu nahisi kwamba Zanzibar tuna fursa nyingi za kuweza kupata mapato zaidi, na kwa mwelekeo huo ambao serikali inaelekeza iweze kuelekeza nguvu zaidi katika ukusanyaji wa mapato yetu ya ndani. Inawezekana sana tukaweza kuongeza makusanyo zaidi na tukaweza kukabiliana na changamoto ambazo ziko ndani ya nchi yetu, katika suala zima la kuwapelekea wananchi maendeleo na wale ambao tunalalamika kuhusu barabara zetu ikafika siku tukafikia mafanikio kuona barabara zetu zinajengwa kwa kiwango cha lami na mambo mengine.

Mhe. Spika, hili lina ushahidi wa kina kabisa, kwamba unapotaka kuangalia katika mazingira yetu unadhani ukiangalia kwa haraka haraka unaona sehemu nyingi sana tuna fursa nyingi za kuweza kuzitumia tukaweza kuongeza ukusanyaji wa mapato zaidi. Lakini kwanza kabisa naomba sana Mhe. Waziri katika kipindi hiki au katika awamu hii tuwe na mkakati maalum na madhubuti.

Mhe. Spika, mkakati wa kwanza tuhakikishe kwanza tunajihakiki, wizara itumie busara zake na maarifa na mkakati maalum wa kuona kwamba tunahakiki watendaji wote ambao wana dhamana katika suala zima la ukusanyaji wa mapato katika nchi hii. Hii itatusaidia sana kuweza kubaini ama zile *gaps* ambazo tunaona kwamba zinaweza zikawa ni *leakage* kwa kupoteza mapato yanayokusanywa.

Nadhani ukweli ni kwamba katika taasisi zetu wamo watendaji ambao wanafanya kazi nzuri, ambao ni wa kupigiwa mfano, lakini tutake tusitake wapo vile vile watendaji ambao hawana nia njema katika suala zima la ukusanyaji. Wanakusanya lakini umakini wao katika ukusanyaji wanaujua wao wenyewe. Hili ni jambo ambalo halifichiki, ni lazima kabisa kwamba Mhe. Spika waziri anayehusika na wizara hii aweze kujitahidi kuona hili tunalisimamia kwa umakini wa hali ya juu.

Mhe. Spika, vile vile naomba sana nimshauri Mhe. Waziri kufanikisha jambo hili, pia kuangalia kwamba, tuangalie kwa kina vyanzo vyetu vya mapato sasa wenyewe, tukitoka katika kuwaangalia watendaji wetu lakini sasa tuangalie vianzio vyetu vya mapato ni vipi ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, viko vyanzo vingi vya mapato ambavyo baadhi yao bado havijasimamiwa vizuri, na kuna vingine bado havijatambuliwa katika kuonekana kwamba vinaweza vikasaidia. Ningeshauri sana Mhe. Waziri hili pia tuliangalie kwa kina. Kwa sababu mpaka sasa hivi unakuta kuna maeneo ambayo yanaweza tukaona kwamba kuna ukusanyaji lakini nguvu bado inawezekana kwamba kwa makusudi ama kwa bahati mbaya bado hatujenda sawia katika suala kama hili.

Mhe. Spika, lakini vile vile ukiachana na hilo tujitahidi katika suala zima la mkakati wa ukusanyaji wa mapato. Mkakati wa ukusanyaji wa mapato ni lazima ufanywe ili kuona kwamba tunaondoa muhali wa namna yoyote. Hapa ndipo ambapo kwa kweli nadhani ni sehemu ambayo moja inayoturejesha nyuma katika nchi yetu. Vyanzo vipo ambavyo tumeweza kuvibaini na hivyo ambavyo hatujavibaini, lakini vile vile tumekuwa na muhali katika suala zima la ukusanyaji. Tumefikia wakati kwamba tunaoneana aibu, tunaoneana haya

kwa njia moja ama nyengine, unakuta kwamba mambo hayaendi kama vile ambavyo yametakiwa yaende.

Mhe. Spika, nikisema hivi kwa mfano. Mimi nilipokuwa nikifanya kazi nilikuwa kama Afisa wa Mifugo wa Wilaya, lakini nilikuwa naona kwamba katika taasisi ile ya sekta ya mifugo kuna suala zima la mfano wa ukusanyaji wa mapato hususan katika masuala mazima ya uingizaji mifugo, na vile vile na katika masuala ya kutoa *permit* kutoka Wilaya moja kwenda nyengine, lakini vile vile katika suala zima la uchinjaji wa mifugo.

Unakuta kwamba muhusika yaani mtaalamu ambaye mwenye dhamana anakwenda yeye mwenyewe kufanya ile kazi, lakini unakuta katika baadhi ya maeneo yeye mwenyewe anaweza akashindwa kuyafikia kutokana na kwamba labda kuna maeneo fulani inachukulika kama ni tishio.

Mhe. Spika, kuna taasisi ya serikali baadhi yao ni kwamba mpaka sasa hivi hawajajua umuhimu wa kukusanya mapato katika masuala kama yale mfano uchinjaji, wanakuwa wanajiamulia tu kwa mfano kuchinja ng'ombe pasi na kuangalia kwamba labda wanalipa kodi na wanakaguliwa vile vile vitu kama hivyo.

Sasa ukiangalia hapa hii fedha kwamba kwa mfano kama msimu huu wa sikukuu tunaokwenda nao fedha nyingi sana pale zinapotea kwenye sekta hii, hizi zingekusanywa vizuri na zikasimamiwa basi nadhani kwa siku ile ya sikukuu tunaweza tukakusanya fedha nyingi sana, lakini sasa kwa watendaji pekee wa sekta ya mifugo ni jambo ambalo kwa kweli hawawezi kufanikiwa na kufikia hayo malengo ambayo tunayatarajia. Nadhani katika maeneo kama haya ni mfano tu angalau wa haraka haraka.

Mhe. Spika, kwa hiyo nadhani Mhe. Waziri sasa ni vyema kwamba kuwe na toleo maalum la taasisi za serikali, kwamba kwa nini mwananchi wa kawaida yeye analipa kodi lakini taasisi za serikali wao hawalipi kodi, inakuwa ni jambo ambalo kwa kweli kwa kiasi fulani hatujaonesha kwamba umakini katika ukusanyaji wa mapato, jambo hili lipo na lipo katika maeneo ya Unguja na Pemba hasa vijijini, mambo kama haya yanakuwa yanatokea. Kwa hiyo ningeshauri sana Mhe. Spika, waziri pia hili nalo alione ni jambo ambalo linaweza likatusaidia. Nimetoa yaani mfano mdogo lakini ukienda hata na kwenye taasisi nyengine mambo kama hayo utayakuta yanatokea.

Mhe. Spika, vile vile ningeomba tu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pia na sisi tuna nafasi katika kuona kwamba

tunalisimamia suala zima la ukusanyaji wa mapato na tukaweza tukapata tozo mbali mbali katika nchi yetu, katika kuona kwamba tunaongeza ukusanyaji wa mapato.

Ushahidi wa hili ni kwamba miongoni mwetu tulio wengi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunakuwa tunakwenda madukani kutumia lakini hakuna mtu anayedai risiti. Ni kweli hata ukiangalia tunapokwenda sheli kuingiza mafuta kwenye magari yetu unakuta mtu anaingiziwa mafuta halafu tena gari inaondoka bila ya kudai risiti.

Mhe. Spika, nadhani sasa tubadilikeni, hii azma ambayo ya serikali basi tuweze kuisaidia na sisi pia tuweze kuisimamia na moja katika lengo la kusimamia ni haya ambayo tunayasema, na sisi tunaishauri serikali iweze kuyafanya haya, tusinunue tu mafuta ya petroli pasi na kudai risiti.

Jengine ningeshauri Mhe. Waziri ahakikishe kwamba sasa tubadilisheni tuwe na kauli mbiu za kuona kwamba sasa kunakuwa na mkakati maalumu wa serikali kuona kwamba ni wajibu wa kila mwananchi na wa kila taasisi kuona kwamba tunaponunua bidhaa mbali mbali hapa nchini kuona kwamba na sisi tunadai risiti ili serikali iweze kupata hizo kodi. Lakini sasa imekuwa ni jambo ambalo kwa kweli, na hili lisiwe ni nyimbo tu, kwamba tuseme tuseme tu kama vile nini, tunamuona Mhe. Rais John Pombe Magufuli jinsi ambavyo anavyosimamia au anavyokuwa na mkakati mbali mbali katika kuona kwamba jambo hili linahimizwa, amethubutu kuzuia hata ajira kwanza kujihakiki kuweza kudhibiti wafanyakazi hewa, kuona kwamba anafanya uhakiki, anaona kwamba hakuna wafanyakazi hewa.

Mhe. Spika, sasa na sisi katika pale ambapo tunaweza tukajitathmini kwa hayo na mambo mengine ya kuwa na mikakati haya yote tunaweza tukabaini kama Zanzibar labda kuna wafanyakazi hewa ama hakuna wafanyakazi hewa, na badala yake tukajikuta kwamba tunaona ukusanyaji wa mapato unaweza kuongezeka zaidi.

Mhe. Spika, naomba nikitoka hapa niende katika mfuko wa barabara *ZRF*. Ninakuwa napata mashaka sana ninapokuwa nikisimama mara nyingi sana hulalamika kuhusu ujenzi wa barabara katika Jimbo langu la Micheweni na kuwa kila bajeti inayokuja nikikuta kipengele cha barabara yaani natamani nifike siku niamue kama Mhe. Jaku kuweza kulia hadharani, kwa sababu ni aibu sana, kwamba ndani ya Jimbo langu la Micheweni ambalo inakuwa moja kwa moja inatoa maliasili nyingi tunazijenga barabara za maeneo mbali mbali hatimaye unakuta kwamba barabara zangu mimi ni mbovu.

Sasa naomba nisiende huko moja kwa moja nikatoka kwenye wizara, lakini niseme tu kwamba nilitaka nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja, nimeona kwamba katika mfuko wa barabara kumejengwa barabara ya Jendele, Cheju, Kaebona na kwengineko huko kwa kiwango cha lami.

Mhe. Spika, hivi nilitaka nimuulize Mhe. Waziri, kwanza wananchi wa Jimbo la Micheweni wamekosa nini, kwamba mifuko yote inayokuja inaelekeza barabara nyengine lakini ukiangalia Micheweni mbona haitajwi, haitajwi barabara za Micheweni unakuta barabara nyengine tu.

Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kwa kupitia mfuko wa barabara pia, kwamba kuona ni vigezo gani vinavyotumika ili hivi vijiji au hizi njia za vijiji ambazo zimetajwa humu zimeingia ambazo zimeikosesha sifa barabara za Jimbo la Micheweni nazo zisiingie katika mfuko huu wa barabara Zanzibar.

Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri, anisaidie, inaniuma sana na inanisikitisha sana, hali ni mbaya na tukiangalia kule kuna viashiria vingi ambavyo kuwa tunasema vya umasikini, kama Wilaya ya Micheweni kuna viashiria vya umasikini basi vimejaa katika Jimbo langu la Micheweni.

Namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kwamba kuvijua hivyo vigezo ambavyo vinatumika katika kuzipata hizo barabara ambazo zinaweza zikajengwa na mfuko huo wa barabara, kama na mimi nina sifa basi niweze kufuatilia nione kwamba barabara za Micheweni zinajengwa.

Mhe. Spika, wananchi wa Jimbo la Micheweni wananiambia mambo mengi kuhusiana na jambo hili na masikitiko makubwa, lakini napiga makelele bado sijaona muelekeo ambao unaweza ukawasaidia, kuona kwamba wanaondokana na hali hii licha ya kwamba naahidiwa ahadi mbali mbali lakini bado sijaamini kutokana na kwamba ahadi kama hizi zinakuwa ni nyingi kwa upande wangu ninazipata.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie katika masuala ya *land use plan* katika Wilaya ya Micheweni ambayo nadhani inagusa inaelekea katika maeneo huru ambayo yametajwa kule katika maeneo ya Micheweni.

Mheshimiwa mimi niishauri wizara kwamba jambo hili ni busara sana ilifanye kwa haraka haraka, lakini pamoja na kufanya kwa haraka haraka ningeomba sana jiografia za maeneo zinatafautiana kwa kila eneo lake husika. Katika Jimbo langu la Micheweni, miongoni mwa mambo ambayo programu nyingi ambazo zimeanzishwa kule zinakuwa zina-*stop*, yaani inakuwa mara nyingi

hazifanyi vizuri, hazifanyi vizuri kwa sababu gani, kutokana na uelewa ambao bado katika Jimbo langu la Micheweni unahitaji tuweze kusaidiana katika suala zima la *awareness*, vyenginevyo tunaweza tukafanya miradi mikubwa na hatimaye tukafikia wakati isiweze kuleta tija katika maeneo yale.

Mhe. Spika, nadhani wizara katika kulifanikisha jambo hili ni vyema watumie wadau wahusika kule katika kuona kwamba inatoa taaluma yakinifu ambayo inaweza ikawapelekea wananchi waweze kujua kiundani na uhalisia na umuhimu wa jambo hili.

Tumeshuhudia miradi chungu nzima inakwama kutokana na uelewa mbaya katika maeneo yale. Kuna miradi kadhaa imekuja kule, nikitoa mfano wakati ilipokuwa inajengwa *community radio* kule Micheweni, kulizuka maneno mengi katika mitaa kutoka sehemu mbali mbali kwamba kule kunajengwa Kanisa, hatimaye ujenzi ule ulikuwa mgumu na ulipelekea kutumia fedha nyingi ambazo zingeweza kutumika katika masuala mengine katika kutafuta dhana au yale *materials* ya ujenzi katika maeneo ya mbali hata yale ambayo kwa kweli yalionekana katika maeneo yale yapo. Na uzoefu wa mambo kama haya katika jimbo langu ni mambo ambayo kwa kweli yapo.

Mhe. Spika, ni vyema sana nimuombe Mhe. Waziri, tutakapoanzisha *project* kama hizi au programu kama hizi basi ni vyema tuone kwamba mkakati mkubwa tunauelekeza katika kutoa taaluma kwa jamii, ili waweze kuyaelewa na wasije wakaona tu kwamba kumefanyika jambo fulani hatimaye tumeshuhudia mambo ya mnara na mambo mengine ambayo umejengwa kwa lengo jema kabisa la serikali, lakini kutokana na kwamba sisi hatujaelewa hasa misingi na ushirikishwaji unakuwa ni mdogo inapelekea mazingira kama hayo.

Ningeomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hili pia nalo aliwekee msisitizo katika kuliangalia suala hili.

Mhe. Spika: Mhe. Shamata muda wako umekwisha.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, na mimi ijapokuwa nina mengi lakini nitayawasilisha kwa maandishi nisikizane na muda, niseme tu kwa niaba ya wananachi wa Jimbo langu la Micheweni na mimi mwenyewe naunga mkono hoja na kuunga mkono bajeti ya wizara hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika: Ahsante sana, sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Maulid Diwani atafuatiwa na Dkt. Makame Ali Ussi na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa fursa hii na mimi kuchangia chochote katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha, iliyowasilishwa na Dkt. Khalid Salum Mohammed.

Awali ya yote napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Jang'ombe kwa kutofanya makosa kwa kunichagua mimi Abdalla Maulid Diwani kuwa Mwakilishi wao katika Baraza hili la Wawakilishi.

Ni mtumwa wa watu wa Jang'ombe na nitawatumikia ipasavyo bila hata chembe ya woga katika maslahi mazima ya watu wa Jang'ombe. Niendelee moja kwa moja katika hoja zangu.

Mhe. Spika, mimi nitachangia moja kwa moja katika suala zima la *TRA. TRA* ni taasisi nzuri sana, inafanya kazi vizuri sana nashukukuru, juu ya watendaji wake walioko pale ni wazuri sana, lakini kuna baadhi ya watendaji hawaitakii mema nchi hii. Nina maana gani kusema hivyo; nina maana kusema kwamba Zanzibar *TRA* ikiwa kama msimamizi wake Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hakuna *uniform* ya *valuation* pale, wanaangaliwa watu kutokana na wewe nani, kipato chako kiko vipi ndio *valuation* zinaendelea, lile ni tatizo.

Kodi nyingi sana ya serikali inapotea kwa kumuangalia mtu, huyu nani kaja na nani anamjua nani. Tunakuomba sana Mhe. Waziri, usimamie hilo suala juu ya baadhi ya watendaji wa *TRA* Zanzibar, sio wote, baadhi ya watendaji wa *TRA* Zanzibar sio wema na hawaitakii mema Zanzibar.

Mhe. Spika, kuna tafauti kubwa sana ya kukadiria mapato kwa bidhaa za aina moja, ni kosa, kama zimewekwa *database* au wanaokubali kulipa asilimia hamsini basi watu wote walipe ile inayotakiwa, siyo huyu analipishwa asilimia hamsini, wengine wanalipishwa asilimia thalathini na ishirini na tano, hawawatendei haki wananchi wa Zanzibar ambao wengi wao ni wakwezi na wakulima wenye kipato kimoja.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, ninakuomba sana kaka yangu, ninajua ni msikivu, muelewa, wewe na Katibu wako Mhe. Khamis Mussa, najua pale alikuwepo anajua kila kitu, lakini nitaomba kupitia sasa kwamba mfanye *operation* maalumu ili kuweza kudhibiti kadhia hiyo.
Pili nitazungumza suala la *ZSSF* (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii)

Mhe. Spika, Mfuko huu umeanzishwa kwa sheria kabisa kuwasaidia watu wetu kwa ajili ya uzeeni, lakini kuna changamoto nyingi *ZSSF*, kutokana kwamba

wanachangia pesa ya mishahara yao na ofisi zinawachangia, lakini hizi fedha hawezi kufaidika mtu mpaka afike miaka sitini, miaka sitini ni mingi sana.

Mhe. Spika, kuna wengine hawamalizi kufika miaka sitini wanafikwa na matatizo mbali mbali, wanaacha kazi kwa namna moja au nyengine, kwa nini haziweki taratibu *at least* wale ambao wanaacha kazi kwenye taasisi ambazo sio rasmi, kwa sababu *private* pia wanachangia pale, *at least* basi wapewe angalau asilimia hamsini ya fedha zao kuweza kujikidhi maisha kwa wakati huo huku wakisubiri hiyo miaka sitini kama watajaaliwa kufika, hilo ni kero, watu wetu wanalalamika sana.

Mhe. Spika, kule kwa wenzetu Bara pindi mtu usipochangia zaidi ya miezi sita miezi saba huna kazi, unakwenda kuomba pesa yako unapewa, kwa nini Zanzibar iwe hawana fursa hiyo. Vile vile hawana fursa hata ya kupewa mikopo, wachangiaji wa taasisi zile wanapeana mikopo wenyewe kwa wenyewe tu, wafanyakazi hawatutendei wema.

Naomba sana Mhe. Waziri, suala la *ZSSF* liangaliwe vizuri juu ya mustakabali mzima wa kuweza kuwasaidia hawa watu wetu, ambao wanaacha kazi kwa namna moja au nyengine bila ya kufika miaka sitini *at least* waweze kupata angalau asilimia hamsini ya pato lao waliloliweka katika *ZSSF*.

Mhe. Spika, jengine nitaingia katika uwekezaji wa PERDUE. PERDUE tatizo jambo mnalibeba sana, kama serikali mnasema kwamba oh! Wazanzibari hawana uwezo wa kuzalisha kuku nyinyi ndio mnasababisha. Ingekuwa kweli tunawapa mitaji watu wetu wa kuja kuwafuga na kuwatafutia wataalamu yule yule wa Perdue akaja Zanzibar akatoa kiasi cha fedha wakapewa wakulima wetu na wafugaji, wakasema tunataka kuku wa kilo moja na nusu kwa pesa hizi hapa inawezekana, lakini kutokana na kuwa mna *interest* zenu katika sehemu hizi nafikiria ndio inakuwa kwamba mnabeba, imefika hatua mpaka kupewa *exemption*, *container* ya kuku inapewa *exemption* kwa misingi gani, inakuwaje *container* ya kuku itoke Marekani mtu atoe bure, je, huyu mfugaji wa kuku ndani atauza vipi kuku wale.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri nakuomba sana hizo barua zipo za *exemption*, hata ukitaka kesho tutakuletea kwa sababu ninazo, na mimi najua hilo kwa sababu mimi nilikuwa *clearing* and *forwading* ninajua kila kitu katika hapo.

Mhe. Waziri, ninakuomba sana juu ya suala zima la uingizwaji wa kuku wa Perdue, naomba tulibane kidogo *at least* watu wetu waweze kufuga ili waweze kuuza kuku wale na wao wajinasue katika giza nene la uchumi mgumu.

Mhe. Waziri nakuomba sana hili suala lisiwe rahisi rahisi tu, japo baadhi ya wajumbe wanapiga kelele perdue wa samaki, perdue ya kuku, lakini inakuwa sawa sawa na kutuletea uporo, hakuna linalokuwa, *still* serikali imelipigia kifua suala hilo. Hamuwatendei haki wananchi wetu walio chini kabisa, wakwezi na wakulima wa nchi hii.

Mhe. Spika, nitaenda katika suala jengine la *AGAPE*. Ni kweli watu wengi sana wamezungumzia *AGAPE*. *AGAPE* ni tatizo, na baadhi ya watu wamepiga pesa nyingi na sijui hatua gani mpaka dakika hii imechukuliwa. Kulikuwa kuna Kampuni tatu zinashindana *tender* katika hii, kulikuwa kuna *AGAPE*, kuna *HUAWEI* na *ZTE*, *ZTE* aliweka dola milioni mbili, *AGAPE* kaweka dola milioni tatu laki tisa na *HUAWEI* aliweka dola milioni nne na ving'amuzi alfu moja bure. Kwa kigezo gani au kwa akili gani kubwa iliyopelekea kuwapa hawa *AGAPE tender* hii ya kusambaza ving'amuzi kuingia katika *digital Zanzibar Television* kwa kampuni hii ya *AGAPE*, wao wenyewe hawawezi, mpaka leo hii nafikiri miongoni mwetu hamna hata mtu mmoja ambaye anayeangalia king'amuzi cha TVZ cha *AGAPE*, ni bilioni nane za wananchi wavuja jasho, wakwezi na wakulima wa nchi hii zimepotea hakuna majibu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, tunakuomba sana utapokuja kwa mapenzi yetu mimi na wewe, uniambie vizuri sana hili suala la *AGAPE*, vyenginevyo vyovyote mimi siungi mkono hoja hata kama mtapiga kura nyote mtakubali, mimi sitokubali mpaka kiama, nitasimamia suala hili, pesa za wananchi bilioni nane si pesa ndogo.

Watu wanalalamika madeksi hamna, barabara mbovu, maji hawapati, baadhi ya fungu la pesa wanapewa watu tu kwa kunufaisha matumbo yao, hawawatendei haki Wazanzibari, tunataka sana Mhe. Spika, hii serikali tunajua makini, na wizara hii makini na ina watu makini, nitaomba sana nipate maelezo ya kina ya suala hili *unless otherwise* iundwe Tume kabisa Kamati Teule kwenda kulichunguza hili suala la *AGAPE*, *AGAPE* ni jipu sio jipu limefika mpaka hatua ya kuwa tenzi sasa Mheshimiwa, Spika.

Mhe. Spika, vile vile ninakwenda katika ujenzi wa *Airport Terminal II. The most expensive terminal in the world*, imetuchukua 128 *million dollars*, ni fedha nyingi sana na mpaka leo *Airport* ile haijamalizika.

Wenzangu wamesema hapa *Airport* ile haifiki hata dola milioni sitini kwa vigezo vyao wanavyovijua, mimi si mtaalamu sana katika ujenzi, lakini mwenye *macho haambiwi tizama*, kusoma hujui basi hata picha huoni, picha tunaona, pesa nyingi sana za Wazanzibari zinapotea hivi hivi tu, na sijui wale

ambao walioitia hasara nchi hii wamechukuliwa hatua gani mpaka dakika hii au kuna taratibu gani zinazofanywa kuwadhibiti wale watu, pesa za wanzanzibari milioni mia moja na ishirini na nane dola ni nyingi sana, sana zaidi ya sana, hiyo tunafanya kufuru, tunasikitika Zanzibar masikini si kweli, Zanzibar ni tajiri, lakini kutokana na watendaji wabovu tuliokuwanao, watendaji wanaojali maslahi yao wanaitia Zanzibar katika majanga haya kuambiwa Zanzibar masikini hatuna uwezo, si kweli.

Mhe. Waziri asimamie sana katika hili na atupe mustakabali mzima wa suala la ujenzi wa *airport Terminal II*, imekuwa hadithi toka mwaka 2009 mpaka leo miaka sita, siku zote hadithi tu *Terminal II* wee, *Terminal II*, sijui lini itamalizika. Nitamuomba sana Mhe. Waziri atapokuja anambie kwa kina kabisa juu ya kadhia nzima ya *Terminal II Airport* ya Zanzibar, vyenginevyo vyote sitounga mkono hoja. Huo ni uamuzi wangu pamoja na wanachi wangu wa Jang'ombe wananisikia nasema haya na wala hawakasiriki katika hilo.

Ujenzi wa Pemba jengo la Wizara ya Fedha ya Mipango halikadhalika. Miundombinu mibovu tunawapa wakandarasi wabovu hawana uwezo, jengo linafikia mpaka kuanguka pesa za Wazanzibari zinapotea, kwa nini tufanye kazi kiholela kama hivyo jamani. Sisi Wazanzibari kwani tumekosa nini kwa Mwenyezi Mungu? Pesa zetu zinapotea, tunawapa wawekezaji hawana uwezo wanakula hizi pesa tu, kulikoni Mhe. Waziri. Nitamuomba sana Mhe. Waziri najua ana uchungu sana alikotoka ni mtoto wa kimasikini wakwezi na wakulima, wamemsomesha amekuwa hapo sasa hivi awasimamie Wazanzibari na Wazanzibari wengi wana imani na yeye asiingie katika kundi la mafisadi papa katika nchi hii. Mhe. Waziri awe msafi asimamie maamuzi yake kila mtu afahamu kwamba kweli Wizara ya Fedha sasa hivi imepata mtu makini wa kuongoza Wazanzibari na kusimamia maslahi yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka niingie katika suala la *ZRB; ZRB* pamoja na kusifiwa sana inafanya kazi vizuri lakini kuna matatizo, kuna *conflict of interest* ambazo ndizo zilizotawala pale. Baadhi ya wafanyakazi wanatoka sehemu moja kama utakuja mfano kulikuwa na mfanyakazi kutoka Zantel *as* Mhasibu kapata kazi *ZRB* kawa *auditor* anatolewa pale aende aka-*audit* Zantel. Jamani wapi tunakwenda, matatizo, mwizi unamwambia ajikamate mwenyewe, ajipeleke polisi mwenyewe, tumeona wapi hayo, tatizo hilo lipo *ZRB* kubwa.

Mhe. Spika, sio hilo tu, wanataja nafasi za kazi hapa Pemba wafanyakazi fulani, Unguja fulani, lakini ikifika *time* hili wanavyoona wao baadhi ya watendaji wakuu wa *ZRB* kumpeleka mtu Pemba kama unamuadhibu, Pemba ni sehemu ya Zanzibar kuna haki lakini basi kuna taratibu maalum

wanapelekana, baadhi ya watendaji wazuri sana wameondoka katika vitengo muhimu sana vya *ZRB* wamepelekwa Pemba kwa ajili ya kukomoana tu. Utanijua mimi nani wewe ulikuwa nani na mimi nilikuwa nani, tuondokane huko Mhe. Spika.

Hilo Mheshimiwa lipo na kero nyingi sana ziko pale mpaka dakika hii kuna baadhi ya taasisi zina miaka minne hazijapeleka ripoti wala hazijakaguliwa kwa sababu ya matatizo hayo ya *interest* za watu. Kuna watu wanajiona kama ile *ZRB* ndio ya kwao, ya baba zao, wakati kile ni chombo cha Wazanzibari, sote tuna fursa sawa katika taasisi zile lakini kuna baadhi ya watu wanajiona wao ndio wao.

Mhe. Waziri namuomba aangalie sana *ZRB* kwa sababu pale ndipo mapato ya nchi hii yanapopatikana. Kuna upotevu mkubwa sana wa fedha na sio hilo tu, imefikia hatua wanakwenda kukusanya kodi kwa *harassment*, wanakwenda katika hoteli na maaskari mpaka kuchukua mabunduki, wapi tunakwenda? Tunazungumza kwamba Zanzibar ni *Paradise Island* leo hii mgeni yuko chumbani anagongewa mlango ukifungua maafisa sita na mabunduki, tunakwenda wapi. Kwa hiyo, wajaribu kutafuta njia za kitaalamu kukusanya kodi waondokane na huku kwenye *harassment* za kukusanya kodi.

Kero zimekuwa nyingi sana, sisi wenye mahoteli ndio wenzetu wawekezaji wanatupa malalamiko hayo. Tumeona nchi gani inakwenda kukusanya kodi kwa mtutu, mkusanyaji kodi na mlipa kodi wanatakiwa wawe marafiki wazungumze lugha moja, wapendane kodi itapatikane. Lakini leo hii unakwenda kukusanya kodi na mtutu wa bunduki unaashiria nini, pana shari pale. Nafasi hiyo *ZRB* inatumia kwa hiyo naomba sana hili suala likemewe kwa sababu wageni wamekuja hapa kustarehe Zanzibar na Zanzibar nchi ya amani, lakini imefika muda sasa hivi wanakwenda kukusanya kodi tu basi wanakwenda na *SMG*, sijui kukiwa na maandamano itakuwaje, maandamano vifaru. Hatwendi huko Mh. Spika.

Vile vile nije na suala la Shamba la Mipira la Kichwele na Pemba. Shamba lile miaka minne sasa wale wafanyakazi hawajui hatima yao, ikiwa kama Waziri wa Fedha ni mlezi wao, kuna watu wanadai mafao yao hata pesa za *ZSSF* ziko pale na yule mwekezaji aliyepewa lile shamba kafikia hatua gani mpaka dakika hii. Kanyang'anywa lakini je, hawa watu ambao wametumikia ile taasisi wamesimama katika njia gani? Tunamuomba atapokuja Mhe. Waziri atwambie juu ya suala zima la shamba la mipira ambalo lilikuwepo hapa Zanzibar (Unguja na Pemba) lakini sasa hivi zaidi ya miaka minne yale mashamba hayafanyi kazi na imekuwa kero kwa wale wafanyakazi waliokuwa katika

taasisi ile kwa kukosa mapato yao. Naomba sana mustakabali wa wale vijana wetu, wananchi wetu, watoto wa wakwezi na wakulima wa nchi hii, wanamapinduzi wananyanyasika katika nchi yao, kwa kweli hatuwatendei haki.

Pia nitaomba ufafanuzi juu ya bodi mbili…

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana, kuna Bodi ya Rufaa ya Kodi na Mahakama ya Rufaa ya Kodi. Mheshimiwa hapa mimi naona kizungumkuti tu Juma unamwita James. Tutamuomba sana Mhe. Waziri katika hili atufahamishe na mwenyekiti wake nani na kachaguliwa vipi. Mazingira mazima yaliyopatikana kwa hii watendaji wa Mahakama ya Bodi ya Rufaa na Mahakama ya Rufaa.

Mengine Mhe. Waziri atakuja kunambia muda nimeshaambiwa hautoshi, nadhani kwa hayo yangu machache kwa kuwa nimetoa mchango wangu katika wizara hii nathubutu kusema kwamba siungi mkono hoja wizara hii mpaka pale nitapojiridhisha na baadhi ya masuala ambayo nimeyauliza kupitia hotuba hii. Nasema ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Waheshimiwa Wajumbe baada ya hapo atafuatia Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi ambae atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassana Juma na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ajiandae, lakini kabla ya hapo naomba nitoe matangazo machache ambayo yapo hapa mezani kwangu.

Tangazo la mwanzo ni la wageni wa Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ni vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevya, *Sober House*. Jumla yao ni 15 na wanaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Polisi, Kheriyangu Mgeni Khamis. Karibuni sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tangazo jengine Waheshimiwa Wajumbe labda nilisome kama lilivyo linatoka kwa Mhe. Nassor Salim Ali (Al-jazira) linahusiana na Timu ya *Kikwajuni Veteran* ambayo nadhani ni timu ambayo iko jimboni kwake inayoongozwa na Mhe. Hamad Yussuf Masauni na Mhe. Nassor Salim Ali, kwamba jana iliifunga timu ya *G1 Mapinduzi Kwanza* inayoongozwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ambae amechangia sio muda mrefu hapa mabao mawili kwa sufuri. Kwa hiyo, alikuwa anasema kwamba timu hiyo ya Kikwajuni sasa

itacheza na timu ya *Baraza la Wawakilishi Sports Club* na mchezo huo utafanyika siku ya mwezi 26 mwandamo wa Ramadhani saa tatu usiku kabla ya mchezo wa *finally* ya *Masauni and Jazira Cup* katika uwanja wa Mnazi Mmoja. *(Makofi)*

Pia napenda niwajuilishe kwamba mgeni rasmi katika mchezo huo anatarajiwa kuwa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar pamoja na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Nape Nnauye. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo sasa naomba kwa heshima na taadhima nimwite Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi ili aendelee na mchango wake. Mhe. Dkt. Makame karibu.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Kwanza kabisa nikupongeze sana Mhe. Spika, kwa utaratibu wako mzuri wa kuendesha Baraza hili. Ni matumaini yangu kwamba tutaendelea vizuri zaidi na zaidi kila tunavyoendelea.

Pili, napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa bajeti hii hapa tuliyonayo nzuri kabisa ambayo imefafanua mambo mengi sana kwa kuzingatia *Programme Based Budget*. Nawapongeza pia wafanyakazi wote akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Wakurugenzi na watendaji wengine wote kwa bidii zao wanazozichukua katika kutekeleza haya.

Baada ya kutoa pongezi hizo sasa na mimi nielekee kwenye hili suala ambalo limejadiliwa sana hapa leo; suala la *AGAPE*, *PBZ*, *Airport* na mengine mengi yaliyozungumzwa. Waheshimiwa Wawakilishi wameonesha masikitiko yao makubwa juu ya uendeshaji wa sehemu hizi na wakapendekeza kwamba iundwe tume itakayochunguza masuala haya.

Mimi sitaki kuzungumzia sana kuhusu *AGAPE*, kuhusu *PBZ*, kuhusu *Airport* yameshazungumzwa, lakini nitasema tu mimi naunga mkono iundwe tume. Kwa sababu kama kuna kosa litaonekana na kama hakuna kosa basi itajulikana hakuna kosa ni fununu tu. Kuna mambo mengine yanaweza kuwa yanazungumzwa, hakuna makosa lakini watu wanayazungumza. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa iundwe tume ili ifanye uchunguzi wa haya.

Pia napenda kumpongeza sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anapopata neno anatwambia. Mimi nafsi yangu nilikuwa sijui kama huko Kijitoupele kuna watu wawili au watatu wamekufa kwa risasi, jambo la kushtusha sana. Kwa kweli hatua madhubuti zichukuliwe baada ya hii...

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa heshima zote naomba nieleze utaratibu, si vizuri Mhe. Spika, kwa Mjumbe kusema jambo ambalo hana uhakika nalo. Sasa mimi nadhani hoja iliyopo mbele yetu ni ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, jambo lolote linalohusiana na masuala ya ulinzi au kitu chochote cha maafa yanayotokana na masuala ya ulinzi taarifa ya kwanza inatakiwa itolewe na Jeshi la Polisi ndipo serikali iweze kusema.

Sasa si vizuri kuja kuchangia hapa ukasema kuna watu wamekufa na ikawa hakuna taarifa sahihi. Kwa hiyo, nimuombe Mjumbe aendelee na mchango wa kuchangia bajeti na hili asubiri Jeshi la Polisi litoe taarifa yake halafu ndipo serikali tuweze kuchukua hatua ya kuweza kutoa taarifa. Nilitaka niseme hilo tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri nadhani hiyo pia isaidie kujibu lile ambalo aliliwasilisha awali Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba sasa serikali inasema tusubiri mpaka Jeshi la Polisi litakapotoa taarifa kuhusiana na hayo matukio, kwa vile mtakapokuwa mnachangia sasa hili liacheni mchangie hoja ambayo iko mezani hivi sasa. Ahsante sana, endelea Mheshimiwa.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa muongozo wako naukubali kabisa na nitaendelea kwenye michango yangu. Kwanza kuhusu hii *budget speech* niseme kwamba ni nzuri na kama ingekuwa ni *thesis* nimeletewa hapa mimi na kama ni mwalimu nisahihishe basi ningeipa asilimia 78, ambayo ni *distinction* ambayo kwa kweli mwanafunzi akiipata asilimia 78 hana upinzani digirii yake anapita tu, wala haulizwi umefanya kosa gani kwa sababu inajulikana kwamba makosa mengine aliyoyafanya yanakuwa ya kibinadamu. Kwa hivyo, juu ya kupita kwa bajeti hii niseme tu kwamba naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Sasa tuingie kwenye Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Spika, tunapozungumzia fedha kwanza nizungumzie fedha baadae nitazungumzia uchumi na baadae tutaingia kidogo kwenye bajeti.

Kwanza tunapozungumzia fedha ni mambo yote yanayohusu mambo ya *banking*, *a leverage*, mambo ya mikopo (*credit*), *capital market*, *money* na *investment*. Pamoja na namna zinavyotumiwa na watu binafsi, serikali au makampuni.

Natoa mchango wangu huu naomba wenzangu wanisikilize kwa makini kwa sababu nitakuja na mapendekezo huko baadae, haya yanayotokana na niliyoyaona kwenye bajeti. Fedha kwa kweli ndio zinazotufanya wanadamu tufanye yale ambayo tunayataka. Tunazalisha mali kwa madhumuni ya kupata fedha tupate chakula, tupate fedha ambayo tutaweka akiba na kingine kilichobaki tupate mambo ambayo hatuzalishi wenyewe. Sasa fedha na uchumi ni mambo ambayo yanakwenda sambamba. Tukienda kwenye uchumi unahusiana sana na mambo ya uzalishaji, usambazaji, mambo ya matumizi ya hizo bidhaa zenyewe na huduma. Hili neno uchumi kwanza linatokana na neno la Kigiriki *economy* ambalo ni *economia*. Kwa hiyo, *economia* Kigiriki maana yake ni mambo yanayohusu jamii, vile vitendo vinavyofanywa na jamii kuzalisha au kuendesha jamii.

Sasa kihistoria au tunapotaka kuujua uchumi kwanza tujue historia ya uchumi, la kwanza hilo. Historia ya uchumi kwanza kuna mambo ya kisiasa, mambo ya u-*Max*, mambo ya uchumi wa aina ya urasimu mpya ambao tunakwenda nao, kuna uchumi wa *canecia*, kuna mifumo na mielekeo mingineyo ambayo imo katika uchumi. Pia inawezekana ikajumuisha mambo mbali mbali yanayoweza kuleta tija katika nchi.

Halafu la pili tunalopaswa kuzingatia ni uchumi wa kiwango cha chini, yaani mimi nauita huu uchumi wa kiwango cha kawaida. Huu unashughulika na mambo ya masoko kuanguka na kupanda, umaalumu, ugavi na mahitaji, mambo ya makampuni, sekta za umma na kadhalika.

Tatu, tuzingatie sana mambo ya uchumi wa kiwango cha juu, haya ni mambo ya ukuaji, mzunguko wa biashara namna inavyozunguka, mfumko wa bei na sera za kifedha. Sera za hazina na urasimishaji.

Halafu kuna ya nne ni uchumi wa kimataifa ambao pia yanaingia hayo niliyoyataja hapo juu.

Nne inakuja uchumi katika utekelezaji, kuna mambo ya nadharia, tukitumia sana nadharia tunaweza tusifike pahala, kuna mambo ya utafiti sasa hapa ndio unatafuta *first finding*, unatafuta ukweli ili uweze kutatua matatizo.

Halafu tena kuna mambo ya taaluma. Sasa mwelekeo unavyotarajiwa ni kwamba tuna sera, tuna kanuni na mambo mengi sana yanayosimamia uchumi, lakini lazima tuweke mkazo kwenye sekta binafsi na hizi sekta binafsi kuna SMEs, kuna viwanda vidogo vidogo vya ujasiriamali wanafanya watu mbali mbali. Sasa hivi tukiweka mkazo mkubwa na vimo kwenye sera huu uchumi wetu hakuna sababu kwa nini usiongezeke.

Halafu mwelekeo mwengine ni juu ya uendeshaji wa uchumi kwa kuzingatia *market forces* na uboreshaji wake. Hizi *Market forces* zinazoonesha uchumi utakuwa namna gani, kama mahala fulani bei za bidhaa fulani zimeshuka na mzalishaji anazalisha kwa wingi twabaan faida atakayoipata itakuwa ni ndogo ukilinganisha kuwa bei zinakuwa ni kubwa.

Sasa katika hili la *Market forces* lazima tujiweke tayari kupambana na *Market forces* kwa sababu bila ya kuangalia hili neno la *Market forces* jinsi linavyoweza kuathiri uchumi tunaweza kuwa tunafanya mambo ambayo hayataweza kutuwezesha kufika mahala popote.

Jengine ni kwamba tulenge kwenye kuwezesha kuleta ushindani katika masoko lazima kuwe na *competition* watu wanaleta bidhaa za nje wanaleta kitu gani. Lakini na sisi tukizalisha bidhaa zenye thamani hizi za nje zinaweza zisipate soko hapa. Lakini pia ni muhimu kuingiza suala la Utawala Bora, tukitumia Utawala Bora makosa mengi haya sijui hapa pameibiwa, inawezekana yakatoweka kabisa.

Sasa katika kueleza hayo lazima tufanye mapitio ya sera zetu mara kwa mara ili ziendane na dhana ya uchumi unaoendeshwa na nguvu za soko. Lazima kuboresha pia na kurahisisha utoaji wa leseni kwa ajili la shughuli hii. Mtu anataka leseni tena sio mwezi mzima anafatilia leseni tu mwisho anavunjika moyo anaacha kufanya *business*.

Pia tuboreshe ufanisi wa huduma zitolewazo na serikali, turahisishe upatikanaji wa mitaji ikiwemo mikopo, tuimarishe miundombinu yote. Kwa sababu miundombinu yote inasaidia katika ulizalishaji, tushirikishe wananchi. Jambo la ushirikishwaji wananchi lazima liwe kubwa sana.

Sasa pia katika uchumi kuna mambo lazima tuyazingatie hususan upande wa *finance*, kuna mambo ya *equity finance* hii lazima tuipe kipaumbele ili tuweze kupata *star fund* kwa ajili ya kuzi-*invest* kwahali kwengine. Halafu pia tuangalie pia kuna *Rocket Scientists* hawa ni muhimu kwa sababu hawa wana ujuzi wa *mathematic* na mambo ya *social science*.

Kwa hivyo, tukiwatumia watu hawa tunaweza tukaongeza uzalishaji kwa maana mapendekezo yao yanaweza yakatusaidia kuendeleza uchumi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana namalizia kuna mambo mengine ya ni *Market equatlity*, kuna *social science* halafu tuangalie pia *bankrupt* tukiangalia mtu aliekuwa *bankrupt* kama utamuwezesha inawezekana akaja juu na kuweza kuzalisha zaidi. Lakini pia inawezekana kumkopesha mtu aliekuwa *bankrupt* ukazidi kuingia hasara na wewe ukaja kuwa *bankrupt.* Kwa hiyo, lazima utafiti ufanyike, ili kujiondolea matatizo haya.

Jengine tuangalie sana *structure row finance*. Baada ya kuzungumza haya haraka haraka sasa niende kwenye kitabu hiki ambacho kwa kweli kimezungumzia sehemu ya mapato na kinaeleza kwamba:

"Mapato yalikuwa ni bilioni mia nane yaliyokusudiwa". Lakini zilizoweza kukusanywa ni nusu ya hizo. Sasa mimi nasema kitengo kizuri kama hicho cha fedha kinapita kinaratibu mambo yake wapi kitakusanya kodi. Nashangaa kwa nini mapato yawe nusu yasifikie asilimia thamanini au zaidi ya hapo.

Naomba mikakati ipangwe ili angalau wanapopanga iweze kukusanya mapato ya kiasi fulani basi yawezekane angalau asilimia thamanini.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ah! Nimekwisha, basi! Basi madhali nimemaliza nisiendelee tena kuchangia ila nasema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia, nawaomba wenzangu wote tuingue mkono hoja hii kwa asilimia mia pia. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi ukanipa nafasi hii nikaweza kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na timu yake, lakini pia nataka nimpe pole kwa kubeba mzigo ambao hakuwa nao lakini ndio majukumu na sisi tuko tayari kumsaidia katika kuhakikisha kwamba majukumu yake anayatekeleza vizuri.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka nianze na ukurasa wa 5 kifungu cha 13 kinazungumzia:-

Katika mapato na moja katika malengo ambayo hatukuweza kufanikiwa ni yale mapato yaliochelewa kutoka *TRA*.

Sasa hebu tuelezwe Mhe. Spika, mpaka sasa hivi kwa sababu hiki kitabu kilivyotungwa kuna miezi kidogo imepita hizi rikodi, sasa hebu tupate *updates* mpaka leo je, yale mapato yaliochelewa kutoka *TRA* kwamba yamepatikana na kama yamepatikana yale makusanyo tutakuwa tumefikia asilimia ngapi.

Lakini pili nataka niwape pole ndugu zetu waingereza kwa mchakato wa kura ya maoni na kuamua kujiondoa katika ile Jumuiya ya Ulaya. Kwa kweli mimi sitaki niwape pongezi lakini nawapa pole kwa sababu naamini katika kipindi kifupi wanaweza wakatikisika kidogo.

Mhe. Spika, nataka niendelee vile vile katika mchango wangu ukurasa wa 10 kifungu cha 4, Mhe. Waziri ameeleza moja katika programu zake ni kuimarisha kitengo cha usimamizi wa madeni. Mhe. Spika, hapa nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri anisikilize vizuri, kwa sababu kitengo hiki cha madeni kwa kweli wao kazi yao ni kusimamia uratibu wa yale madeni. Lakini pia nilikuwa namuomba Mhe. Waziri awe mkali sana na awe karibu sana na kuangalia haya madeni tunayapata vipi.

Mhe. Spika, kuna madeni mengine wakati mwengine tunayapata kwa uzembe. Juzi kuna Mheshimiwa mmoja aliambiwa aombe radhi kwa kusema uzembe. Lakini uzembe unapokuwa uzembe hauwezi ukawa sio uzembe, uzembe bado utaendelea kubakia kama uzembe. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ukiangalia katika hayo madeni mimi umenipa nafasi ya kuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na nimekuwa Mwenyekiti katika kipindi kifupi nimegundua serikali inaingia madeni bila ya sababu za msingi. Nimejaribu kuangalia na huyu Mkandarasi ambae amejenga barabara zile za Pemba; Wete- Gande nafikiri na Wete-Chake. Mhe. Spika, ukiangalia bajeti sisi ndio tunaopitisha hapa tunaingiza fedha za *compensation* na yule *contractor* tayari ameshakabidhiwa *site* anafika pahala karibu miaka mitatu *compensation* haijalipwa. Kwa hiyo, ina maana serikali inaingizwa madeni ambayo yanakuwa hayana msingi na Mhe. Spika, tulipojaribu kuzungumza na yule muwekezaji ameshahangaika serikali nzima; ameshakwenda mpaka kwa Makamu wa Pili wa Rais lakini mpaka leo anapigwa danadana huku na huku.

Hebu sasa serikali itwambie huyu mjenzi kweli kama kuna pesa zake anadai apewe haki yake ili aendelee na shughuli na nyengine. Lakini sio hivyo tu

tuangalie na mfuko wa barabara. Mhe. Spika, yaani hapa serikali siku zote wanaposema hawana pesa ndio maana mimi nakuwa mkaidi sikubali, kwa sababu kuna fedha zinatumika ovyo ukiangalia sisi baada ya kwenda Pemba tumejaribu kufanya utafiti kuna barabara ile iliyojengwa kule ya Meli tano Madenjani.

Yule mjenzi kipindi kile alikuwa *additional work* ya kuendelea na kazi nyengine wakakubaliana na wizara ile kutoka Madenjani mpaka wanaita Mzambarauni ilikuwa kama kilomita tatu au nne. Mhe. Spika, yule mkandarasi walivyokubaliana Wizara ya Mawasiliano akakubali kufanya ile *extension*, kwa shilingi bilioni moja na milioni mia mbili. Mfuko wa barabara wakakaa ushauri wa wataalamu wa Wizara ya Mawasiliano matokezeo yake Mfuko wa barabara wakasema iitishwe upya *tender* ili ile kazi iweze kushindaniwa.

Mhe. Spika, cha kusikitisha yule mkandarasi anasema ikiitishwa *tender* hizi gharama zitaongezeka. Matokezeo yake imeitishwa *tender* yule yule mkadarasi ikabidi *tender* karibu bilioni mbili na akasema kuna *crash* ya serikali apewe bure lakini matokeo yake ikawa karibu bilioni mbili na ile kazi ikawa tayari wameshapewa wakandarasi. Sasa Mhe. Spika, hapa kuna karibu milioni mia nane zilikwenda tu hivi hivi, sasa hili nina wasi wasi na barabara ya Fuoni.

Barabara ya Fuoni sisi tumetembelea Mhe. Spika, wananchi wanapiga kelele mmoja katika muathirika mkubwa Mhe. Abdalla Maulid Diwani siku zote gari yake akija hapa Barazani inaandikwa kosha gari, akikosha gari akifika Fuoni gari imechafuliwa, akirudi anandikiwa kosha gari. Mhe. Spika, barabara ile inakwenda vizuri ilikwama pahala fulani tayari wameshakubaliana wizara na yule mjumbe kwamba *extra work* nafikiri aongezwe karibu bilioni tatu ili aweke lami.

Kitu cha kusikitisha juzi Mhe. Waziri alipokuja anasema imeitishwa *tender* upya sasa nina wasi wasi baada ile bilioni tatu iliokuwa ya ofa na yule mkandarasi inawezekana ikawa bilioni saba hiyo *tender* ya lami. Sasa hiyo, Mhe. Spika, ndio maana tukasema kwamba serikali wakati mwengine inaposema haina pesa tunakuwa hatuko makini katika kusimamia ile mipango yetu, taasisi zishirikiane mfuko wa barabara, Wizara ya Miundombinu ni baba mmoja mama mmoja seriakli ndio hiyo hiyo, isiwe Wizara ya Miundombinu anaamuwa hivi na Mfuko wa Barabara unakuja kufanya maamuzi mengine. Tunaingiza hasara serikali bila ya sababu yoyoye.

Hili naomba hebu aliangalie Mhe. Waziri, nina amini ile bilioni tatu ambayo ilikuwa ofa na yule mkandarasi sijui kama haitofika bilioni saba kwa ajili ya

kukamilisha lami. Wakati Mhe. Spika, utaratibu huu unakuwa unafanyika mfano wenzangu wamezungumza *terminal II*, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano lakini sijaridhika kabisa Mhe. Spika, tulimkamata sana hapa aliekuwa Waziri wa Mawasiliano kipindi kile Mhe. Hamad Masoud kila siku alikuwa anatubabaisha maana yake *designing building* matokeo yake mpaka leo jipu lile pale limetukalia chini. (*Makofi*)

Lakini pamoja na yote Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, fedha za kumalizia *terminal II* azitowe, mimi sina tatizo kuundwa kamati teule kama Waheshimiwa wanataka waende wakajue lakini fedha hizi kama hazikutolewa Mhe. Spika, lile dude litakuja kuwa mara kumi zaidi gharama kila siku zinapoongezeka. Suala la kuundwa Kamati Teule Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa wameshajenga hotuja wacha Mhe. Spika, ufanye maamuzi yako lakini mimi naomba ujenzi wa *terminal II* fedha ziingizwe ile lile, dude tulitumie, wenzetu Bara wamejenga juzi kesho kutwa wanatupita. (*Makaofi*)

Mhe. Spika, suala la *AGAPE* tulimkamata koo hapa Mhe. Said Ali Mbarouk Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk, Mhe. Hamad Masoud yalikuwa majipu yametutia hasara. Mradi wa *AGAPE* hapa na mimi Mhe. Spika, nakubaliana iundwe Kamati Teule twende tukachunguze na mimi sitokubali kuruhusu kutoka fedha nyengine kuendeleza mradi ule kama hatujapata uhakika wa matatumizi na kama kuna watu waliwajibika ambao waliofanya ubadhirifu wawajibike, Mhe. Rais kasema yeye hatumbui majipu atatoa jipu mpaka moyo, tunataka tuone moyo katika *AGAPE* na *terminal II.* (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikiendelea nilikuwa nataka tu nijue hii misamaha ya madeni, kuna kampuni mbali mbali; kuna viwanda mbali mbali kuna kiwanda cha sukari, kuna kina kiwanda cha maziwa hebu tupate hii misamahaa imepatiwa kiasi gani. Lakini narudi katika suala la *perdue* Mhe. Spika, jana nilisema nilitoa angalizo kwa Wizara ya Fedha tunataka tujuwe kodi wanaolipishwa kuku wa *perdue* na haya masamaki mapya sasa hivi yaliyoingia Zanzibar tunataka tujue kodi yake inalipishwa vipi na ile *rate* wanaangalia vipi huko duniani.

Vile vile Mhe. Spika, nakuja suala la *ZIPA*. Mhe. Spika, *ZIPA* hebu naomba leo Mhe. Waziri aje anieleze ule mradi wa yule muwekezaji anaetaka kuweka chekelezo yule Mzanzibari umekwama wapi. Mhe. Spika, ile .....

Mhe. Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma utakuja kumalizia dakika zako tano zilizobaki naomba sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti ili aje anipokee. Mhe. Mwenyekiti, tafadhali.

(*Hapa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Suala la *ZIPA* leo tukiangalia hii mitikisiko ya uchumi duniani nchi kubwa kubwa leo zinakuwa hazielewani, hazitambuani, tunatakiwa tuwape nguvu wawekazaji wa ndani. Leo kuna muwekezaji amejitolea mzalengo na Mhe. Waziri Fedha aliepita tulikubaliana hapa hebu tukakae na Mhe. Waziri wa Fedha kuna sababu gani yule ndugu yetu mpaka leo wakawa hawataki kumpa hatimiliki au kumpa *lies* kuendeleza ule mradi wake.

Leo tunapenda sana kutengeneza makampuni ya nje kuwapa fedha makampuni ya nje wawekezaji wa ndani Mhe. Spika, tunawadharau. Hii kwa kweli inarudisha nyuma sana. Hili nilikuwa naomba Mhe. Waziri kwa sababu Kamishna wa *ZIPA* analijua vizuri watakapokwenda kukaa akae vizuri waje wanielezee vizuri na maneno yasije kubadilishwa, nisije kupewa jawabu kama kipindi kile kilichopita.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile *ZIPA* naomba sana juzi nilizungumza kuna muwekezaji wa *Penny Royal* kule Nungwi; mpala leo anawanyanyasa wananchi amechukuwa maeneo yao wanashindwa kulima lakini mpaka leo anashindwa kuwalipa *compensation*. Vile vile Mhe. Spika, wamenituma wananchi wa Fumba. Wananchi wa Fumba wamechukuliwa maeneo yao na wawekezaji sasa hivi hawawezi kulima, hawawezi kufuga, mpaka leo hawajalipwa *compensation.* Hebu naomba Mhe. Waziri akija vile vile aje anipe taarifa za wananchi hao.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia suala la *PBZ,* kwa kweli wanafanyakazi nzuri ingawa kulikuwa kuna matatizo kidogo majipu na baadhi yao yametumbuliwa. Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali kazungumza vizuri, kwa hiyo hili nafikiri ni kazi ya kiti cha Spika aangalie. Lakini nilikuwa naomba leo *PBZ* na taasisi nyengine za serikali mfano kama Shirika la Bandari ni baba mmoja mama mmoja.

Shirika la Bandari ni Shirika la Serikali na *PBZ* ni Taasisi za Serikali leo haiwezekani Shirika la Bandari lina matatizo wanakwenda kukopa pesa *PBZ* wanashindwa kuwapatia. Kwa kweli hili suala sio zuri sana. Naomba sana tumezungumza sana Bandari sasa hivi kuna *congestion* ya makontena, vifaa hawana wanataka kununua *spears.* Leo kweli Shirika la Bandari, *PBZ* watafurahi kuona wanakwenda kukopa katika benki nyengine, kwa kweli hili

nilikuwa naomba sana Taasisi za Serikali wakati wana uwezo wa kulipa wasaidiane.

Mhe. Mwenyekiti, soko la Bima la Zanzibar kwa kweli nalipongeza sana. Moja katika malengo yao waliotuletea mwaka uliopita wameweza kuyavuka. Sasa hili nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri hebu akija aje anisaidie juzi nilizungumza nae kwenye simu lakini kwa bahati ikawa ile *issue very agent*, kwa hiyo nikajaribu na mimi mwenyewe kuifatilia.

Tulizungumza na Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano kuhusu suala la kauli aliyoitoa Bungeni kwamba Taasisi zote za Bima zikate Bima kutoka Shirika la Bima la Taifa. Kwa kweli Shirika la Bima la Zanzibar ni Shirika la Taifa vile vile kwa sababu ni Shirika la Serikali na wao wameekeza Zanzibar, wameekeza kule Tanzania Bara na miongoni mwa mapato yao asilimia kubwa wanapata kutoka Tanzania Bara.

Sasa kauli ile ya Waziri wa Fedha kama hatukuingilia kati ikarekebishwa, ili zile taasisi za umma isiwe kwamba wakate Bima au watumie Bima zao kupitia Shirika la Bima la Taifa, lakini iwe mashirika ya Bima ya Serikali. Na Katiba zetu zote mbili zinatambua; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *ZUSP*. Mhe. Mwenyekiti, bado ninarejea tena na ninamuomba tena Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, mara tu baada ya kupitisha bajeti hii, naomba aweze kuwalipa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura na Shaurimoyo, kuhusu *compensation* kwa ajili ya kujenga ule mtaro. *Otherwise* zikichelewa hizi pesa nina wasi wasi isije ikawa ikaongezeka zile *extra work*, ikaja ikaongezeka gharama kwa ajili ya ujenzi ule, ikaja ikawa bajeti tumeipitisha ikawa inaongezeka matumizi kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka ninawapongeza sana na kwa kweli wanatoa wataalamu wazuri na hata maendeleo ya Chuo cha Chwaka ukiangalia kipindi cha nyuma na sasa hivi, kwa kweli yapo tofauti sana.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 28 wa kitabu cha Mhe. Waziri ameeleza kwamba kuna suala zima la kulipa malipo ya kiinua mgongo. Lakini bado nilikuwa namuomba tena Mhe. Waziri bajeti tunayoipitisha ni bajeti ya *PBB*. *PBB* kama tutaendelea kuwa madeni ya nyuma, *PBB* inakuwa haitekelezeki, kwa sababu tunapitisha bajeti ambayo haina uhakika wa utekelezaji wake. Kwa hivyo pamoja na madeni ya viinua mgongo ya walimu pamoja na pesa zao za

likizo ambazo sasa hivi zinakwenda karibu bilioni nne, lakini kwa bahati nzuri tuna fedha siyo ya kutosha lakini tuna fedha si haba, karibu bilioni thamani na tatu hivi zimetengwa kwa ajili Mfuko Mkuu wa Serikali na miongoni mwao itakuwemo katika kulipa haya madeni.

Sasa hapa nilikuwa naomba vile vile suala la kiinua mgongo watakapokuwa wanaangalia utaratibu, basi liangaliwe na kupunguzwa hadi kumalizwa kabisa suala la deni la walimu. Kwa sababu wengine wameshakufa sasa hivi, wengine wameshastaafu wanahangaika na maisha. Unajua unapokuwa serikalini, ukitoka nje ya serikali kwa kweli unaanza kupata kizunguzungu na kama ukikosa pesa zako kwa wakati Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli unaweza *paralysis* au ukapata maradhi mbali mbali ikiwemo sukari.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Manunuzi. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwa Mhe. Waziri na humu nimeona katika mpango wake, naomba tuiangalie sana Sheria ya Manunuzi. Sheria ya Manunuzi wakati mwengine inatutia hasara wakati mwengine kitu ambacho cha shilingi kumi kinafika shilingi hamsini kwa kufuata Sheria ya Manunuzi. Tunaomba Sheria ya Manunuzi ije, tuifanyie marekebisho. Wenzetu Tanzania Bara hii wameiona wameshaanza kufanya marekebisho ili kuhakikisha kwamba fedha hii *PBB* iende vizuri, basi kuwe na ubanaji wa matumizi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ameeleza Mhe. Waziri kuna ujenzi mbali mbali wa barabara ikiwemo barabara ya Cheju. Juzi nilisikia taarifa kwamba serikali imevunja mkataba na ile Kampuni ya SHAPRIA. Lakini kuna watu chini chini wanaiendea mbio Kampuni ya SHAPRIA iendelee kupewa tena kazi. Mhe. Mwenyekiti, kampuni ile kwanza hao walonipa *tender* sijui walikuwa wanasinzia au wamelewa. Kampuni haijawahi kufanya kazi pahala popote ya ujenzi ya barabara. Leo wamekuja kuipa kampuni kujenga barabara, barabara imewashinda na wamekimbia. Sasa leo watwambie serikali hatua ya mjenzi huyu imefikia wapi na kama kuna mali zake zikamatwe na kama kampuni ishitakiwe watulipe pesa zetu. Hatuwezi tukawa kichwa cha mlezi, watu wanakuja kujifundishia kunyoa hapa na hawa Wajumbe wa *Tender Board* wanapotoa hizi *tender* wafuatilie uzoefu wa makampuni, historia ya makampuni wasituletee tu hapa makampuni ya mfukoni. Kila mtu anaranda na kampuni yake mfukoni. Tunataka *experience* ili tunapotoa kazi tuhakikishe kwamba kazi tunayoitoa ina uhakika. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninamalizia naona ushaanza kunitazama tazama na hii ni Ramadhani. Mhe. Mwenyekiti, suala la *TRA*. Ninamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha mutakapokuwa katika vikao vyenu, bado tujenge hoja kuwa *TRA* ni

chombo cha muungano. *TRA* mpaka leo sisi Zanzibar kuna Makamishna wanne, wote wanatoka Tanzania Bara. Zanzibar nzima tuna Naibu Kamishna. Naibu Kamishna hawezi kufanya maamuzi zaidi ya yale ya Makamishna wake.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, siku zote tutaendelea kulalamika Waziri wa Fedha ya Jamhuri ya Muungano anaposoma bajeti yake, atatangaza makodi mbali mbali, huku Waziri wa Fedha anazungumza kuwa bajeti yetu safari hii hatuongezi kodi, lakini kuna kodi *automatic* akizitaja kuziongeza Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano na hapa Zanzibar zinaongezeka vile vile. Kwa hivyo, naomba sana suala la Kamishna wa *TRA* lazima Zanzibar tupate Kamishna wa *TRA*. Wenzetu Bara leo Mkoa wa Morogoro wana Kamishna. Zanzibar nzima hatuna Kamishna. Kwa kweli hili suala siyo zuri. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninamalizia suala la *BOT* dakika moja yangu iliyobakia. Mhe. Mwenyekiti, suala la *BOT* bado nitaendelea kusikitika nalo. *BOT* mpaka leo Zanzibar tumeendelea kutoa Naibu Gavana. Miaka sasa hivi ni zaidi ya hamsini ya muungano bado Zanzibar, kweli hatuna wataalamu, hatuna wachumi wanaoweza kuwa Magavana wa *BOT*. Na hili bado tunaendelea kulipigia kelele, tutaendelea kupiga kelele.(*Makofi*)

Lakini leo Mhe. Mwenyekiti, huyo Naibu Gavana tuliyekuwa naye, sasa hivi pia ameshapunguzwa nguvu. Kuna Manaibu Magavana wengine sijui wawili, sijui watatu. Yaani kila siku sisi tunakwenda chini chini mpaka lini Mhe. Mwenyekiti. Sasa hivi tunataka hao Manaibu Kamishna wakiongezwa kule Tanzania Bara, basi na hapa waongezwe lakini zaidi tunataka nafasi ya Ukamishna tupewe.(*Makofi*)

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi sisemi nitaunga mkono kwa asilimia ngapi, kwa sababu kuna maamuzi ya kiti chako ninayasubiri ili baadae niweze kuipitisha hii bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza kwa mchango wako mzuri. Sasa hivi ninamuomba Mhe. Hassan Khamis Hafidh akifuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Said Omar Said ajitayarishe.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninapenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana na mimi kunipatia nafasi hii ya kuwa mchangiaji katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yangu, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Welezo, kwa niaba ya wakulima na wakwezi wa nchi hii naomba kuchangia kwa lengo moja tu, lengo la kuimarisha maendeleo na kuondoa umaskini Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hii ndiyo wizara yenye mambo yote kwa sababu ina-*deal* na mambo wanayoyapenda watu wote duniani, fedha. Bila ya fedha hatuwezi kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kumkumbusha Mhe. Waziri usemi wa Hayati Baba Madiba Mandela alisema, *poverty is a man made*. Kwa msingi huo kama *poverty is a man made*. Ni sisi wanadamu ndiyo tunaosababisha umaskini. Aidha, kwa familia au taifa.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ni Zanzibar. Ni nchi ya kimapinduzi, ni nchi changa, ni nchi maskini. Wanapokuwa wanajitokeza wajanja wachache wakaanza kuiba kwa maslahi ya ubinafsi wanalitia taifa katika matatizo makubwa. Maafa yanayopatikana katika mahospitali kunakuwa hakuna madawa, wanafunzi wanakosa kwenda skuli, wanakosa elimu bora kwa manufaa yao binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, naanza mchango wangu kwa wizara hii. Wizara hii kuna mfuko wa wafanyakazi ambao wafanyakazi katika taasisi mbali mbali za serikali wamekubaliana kuwa na mifuko mengine kama *SACCOs*, mifuko mengine ya ufiwa na mifuko mbali mbali ambayo wafanyakazi hao wamekubali wakatwe mishahara moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha iende katika mifuko yao. Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu Wizara ya Fedha, pesa hizo zinakatwa lakini hazifiki kunakohusika na pesa hizo kuna tetesi zimeshaibiwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema wazi wazi baadhi ya *documents* za wizi ninazo. Wizi huo umetokezea upo na huo wizi ni jipu, kwa sababu watu hao wapo. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anapokuja aje kutujibu watu hao ni kina nani na wameiba kiasi gani na kwa nini wameiba. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia nitakuja katika agenda yangu namba mbili kwenye *airport*. Mhe. Mwenyekiti, siyo siri nchi nyingi za Kiafrika zinashindwa kuendelea zinapoanza *projects* kwa sababu watu wengi wanakuwa na *self interest*, wanakuwa wanataka kuiba. Kila mtu ana tamaa doo! Mradi huo sasa nitakula, mradi huo sasa nitatajirika. Mradi wa *airport* mimi ninathubutu kusema *the most expensive terminal* kujengwa *over the world* ni ile *terminal II*. Pesa zilizotumika pale ni nyingi. Pesa ambazo tumefanya *research* tumegundua

terminal chungu nzima zimejengwa haziwezi kufikia pesa kama zile. Pale Mhe. Mwenyekiti, pana wasi wasi wa wizi, pana wasi wasi wa watu kuiba, kula pesa hizo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili tukumbuke ni Baraza la Tisa tumekuja humu na nia moja tu ya kuja kuwaokomboa wanamapinduzi, kuyadumisha na kuyaendeleza mapinduzi matukufu kwa kuwatetea wanyonge na wakulima. Mhe. Mwenyekiti, tutawatetea kwa njia yoyote ile tukiwa Barazani, tukiwa nje ya Baraza. Tumekubali kwa dhati kabisa kuwafichua wale wezi wote na wanaodhulumu mali ya umma, tutawafichua na kuwasema usiku na mchana na serikali tunaiomba ichukue hatua. Hatutawaachia kuendelea kukitia doa Chama chetu cha Mapinduzi kwa maslahi yao binafsi. Tutawafichua, tupo tayari kwa vyovyote tumejipanga dhidi ya wale wote wanaokichafua Chama cha Mapinduzi na serikali yake. Mhe. Mwenyekiti, *airport* pameibiwa pale *terminal* ile tunaomba zichukuliwe hatua. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninakwenda katika *AGAPE*. Bila ya siri Mhe. Mwenyekiti, katika watu waliokuwa *proposed* kupata *tender*, *AGAPE* walikuwa hawamo. Lakini wametokea wajanja wachache kwa maslahi yao binafsi kwa kutaka kuiba na kudhulumu mali ya wakulima na wakwezi wa nchi hii *AGAPE* wameiingiza. Wataalamu walishauri *AGAPE* haifai. Kamati ya Wanasheria walishauri *AGAPE* haifai, haikupitishwa katika Baraza la Makatibu Wakuu. Mradi huo ulikuwa hauna uhakika kwa sababu ile kampuni haijulikani. Mhe. Mwenyekiti, mpaka leo hatuna *case number* ya mradi huo. Mhe. Mwenyekiti, mpaka leo serikali ilitakiwa kupata asilimia 60 haijapata. Ving'amuzi havina viwango. Mhe. Mwenyekiti, ni wazi kabisa kwamba mradi ule tumeingizwa hasara kwa maslahi ya wachache, wezi, wa mali ya wakulima na wakwezi, wanyonge wa nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo Kanuni ya 120 inampa uwezo Mhe. Spika ya kuunda Kamati Teule. Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taadhima kubwa tulimteuwa Mhe. Spika kwa kumjua ataweza kuwatetea wanyonge na wakulima. Tunamuomba sana atukubalie maoni yetu sisi wakulima na wakwezi kwa kuunda Kamati Teule ya kwenda kuchunguza wizi huu walioibiwa wakwezi na wakulima wanyonge wa nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, tupo tayari kwenda kuchunguza na tukiwapata wizi hao tutawaleta hapa, tutawafichua kwa maslahi ya wanyonge na wakulima wa nchi hii.

Ninaamini kwa wizi huu, dhuluma hii kwa wakwezi na wakulima kiti chako cha Spika hakitotuangusha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yangu, wanachama na wananchi wa Jimbo la Welezo wakwezi na wakulima wa nchi hii tunaomba kwa dhati Kamati Teule leo hii iundwe. Mhe. Mwenyekiti, kuna kadhia ya *PBZ* yote iingie kwenda kuchunguzwa wizi huu waliodhulumu wakwezi na wakulima wa nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili la Tisa limedhamiria kwa dhati kabisa kuwafichua wizi wote wa nchi hii kwa maslahi ya Chama cha Mapinduzi na serikali yake inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein muungwana wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona mfano wa Rais wetu jinsi gani alivyong'ang'ania maendeleo ya nchi hii. Hana tamaa, hakupata kuiba cha mtu. Kwa nini baadhi ya watendaji na wakubwa wa nchi hii waibe. Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili la Tisa ndiyo jawabu ya hiyo tutawafichua na tutakwenda nao sambamba. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo Wizara ya Fedha jana walikuja na kauli nzuri hapa ya kusema anaahidi kubana matumizi na kukusanya *taxes*. Nilipokuwa nikichangia nilisema Mhe. Mwenyekiti, yeye ndiye mwenye kila kitu. *ZRB* ina kazi nyingi, ina kazi ya kukusanya, ina kazi ya kuwatafuta wasiolipa, ina kazi ya kuwashitaki wasiolipa, ina kazi ya kuwatafuta wasiolipa kwa wakati. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kwa hili awapunguzie kazi, wafanye kazi ya kukusanya tu *taxes* na iundwe taasisi nyengine ije na jukumu la kuwatafuta na kuwashitaki hao wengine. Ili kuwapa ufanisi *ZRB* katika kukusanya *taxes*. Ni wazi kwa sababu ya kufanya mambo haya yote pana *conflict of interest* katika idara mbali mbali ndani ya *ZRB* ambayo inasababisha uvujaji mkubwa wa mapato ya wanyonge na wakulima na wakwezi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, suala la risiti. Suala la risiti ni suala zuri inapendeza. Nchi nyingi duniani wanazitumia na wamefanikiwa lakini kama hatujawa *serious* katika suala hili la kumkamata asiyetoa risiti, asiyelipa *taxes*, tukamleta mbele ya watu; asiyetoa risiti, asiyelipa *taxes* tukatumia *formula* ya Uingereza *Name and shame*, halafu tukamshitaki hatatofanikiwa. Ni suala zuri na risiti lazima iwe na *TIN number*. Lakini kama hatujalisimamia kwa dhati watu watatumia pesa kununua vimashine bila ya tija. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuna Shirika la Bima ambalo lipo chini ya Mhe. Wizara ya Fedha na Mipango. Mhe. Mwenyekiti, watu wote wenye magari katika nchi hii wanasababisha ajali kila siku hasa wenye daladala, wanatuulia watu wetu kila siku. Mhe. Mwenyekiti, ninakuomba dunia nzima Bima inamlinda mpaka mwenda kwa miguu, inamlinda abiria na taasisi hiyo ianzishe utaratibu wa kumlinda mwenda kwa miguu, ianzishe utaratibu wa kumlinda na abiria. Mhe.Mwenyekiti, nitatoa mfano daladala anamgonga mtu, baada ya siku tatu

anakuwa nje anatembea aliyemgonga mtu, ameshamkata uti mgongo ameiachia familia yake, yeye na gari wanafanya biashara anampelekea soda na mboga ya mchicha siku halafu anaingia mitini. Mhe. Mwenyekiti, kwa hilo hatuwezi.

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa jengo Pemba. Wizara ya Fedha imeomba pesa kujenga jengo Pemba. Jengo Pemba lipo lakini bovu. Ni wazi kwamba pale mkandarasi hakufanya kazi au wamepeana *tender* hiyo kwa kujuana kwa kupata kitu kidogo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza aje atujibu kuwa lile jengo la Pemba mkandarasi huyu kama wameitia hasara, atarejeshaje pesa za wakwezi na wakulima, lazima zirejee. Kama si hivyo Mhe. Mwenyekiti, hapa itakuwa sasa tunaitia serikali hasara kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Chuo cha Fedha kinafanya kazi uzuri lakini chuo hichi kinasikitishwa na kutolipwa na serikali. Chuo cha Fedha kinaidai serikali milioni mia sita. Ninamuomba sana Mhe. Waziri jembe alishughulikie hili, chuo hiki kilipwe.

Mhe. Mwenyekiti, maslahi ya wafanyakazi wa Chuo cha Fedha wanafanya kazi mpaka usiku na hawalipwi malipo ya ziada kitu ambacho kimo ndani sheria.

Mhe. Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wa Wizara ya Fedha pia wameomba kuongezewa mishahara, hawajaongezewa. Mhe. Mwenyekiti, ninataka Mhe. Waziri aje anijibu barua hii ya kuomba Utumishi kuongezwa mishahara hawajaongezewa mpaka leo ipo wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Mfuko wa Barabara. Mfuko wa Barabara huu ninaomba sana ukae upange na uangalie kitu kinachoitwa Wilaya ya Magharibi "A" na "B". Mhe. Mwenyekiti, si siri Wilaya hizi kuna watu wengi lakini miundo mbinu ya barabara hakuna, mji umekaa vizuri kule, kule kumekaa vibaya hakuna barabara. Mhe. Mwenyekiti, naona umewasha taa yako na mimi ninaendelea kuwatetea wakwezi na wakulima, naomba sana Kanuni ya 120 leo Baraza hili la Tisa, Baraza la mkomboa mwananchi wa Zanzibar mwana mapinduzi, Baraza la kumkomboa mkwezi na mkulima lipitishe na likubali kuteuwa Kamati ya kwenda kuchunguza kadhia hii ya wizi ya Wizara ya Fedha, pesa za wafanyakazi, *PBZ, airport, AGAPE.*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba sana uridhie. Naomba kusema ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hassan. Sasa ninamwita Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Said Omar Said na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe katika mchangiaji katika Wizara ya Fedha na Mipango.

Sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na afya njema nikaweza kusimama hapa, naomba Mwenyezi Mungu anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu, na pia niwapongeze watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango, kwa kazi yao kubwa waliyoifanya ya kutayarisha kitabu hiki ambacho ndio roho ya serikali. Kabla sijachangia kupitia kitabu hiki, nina mchango maalum kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, naomba ausikilize sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, umepewa jukumu kubwa sana pahali ambapo pana bilisi, kwenye fedha pana bilisi, kwa hivyo, uwe makini. Wewe mwenyewe kwanza nakuomba utosheke, kwa sababu kuna msemo huu unasema kwamba; 'Kila mwenye kutaka utajiri kukinai kunamtosha'. Sasa wewe mwenyewe ukishakinai basi utaweza kutekeleza majukumu yako, haitakuwa bora kwamba wewe umeshaona majipu yaliyotokea hapo, kila mmoja anatajwa alipokuwa Wizara ya Fedha na wewe ukaunga mkono hali hiyo hiyo. Nakuomba sana utosheke, hapo ndipo utaweza kufanyakazi zako.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye mchango wangu wa mahitaji ya kitabu hiki kama ilivyo. Usimamizi wa Mahitaji ya Umma, kuhusu ukamilishaji wa jengo la Ofisi ya Rais, Katiba na Sheria Utumishi. Katika kitabu hiki Mhe. Mwenyekiti, ilionesha kwamba wizara itakamilisha jengo hili, jengo kwa nje tunaliona kwamba limekamilika. Naomba atakapokuja atueleze kwamba jengo hili kukamilisha vipi na katika kukamilisha huko ni ujenzi ama ni hatua za mwisho zilizobaki, kwani jengo hili lilikuwa ukiingia mule ndani ni kama kaburi, jengo kubwa kama lile halina *AC*. Sasa ukamilishaji huo ni pamoja na vitu kama hivi, ili wafanyakazi waliomo mule waweze kufanyakazi kwa utulivu kabisa, hali iliyokuwepo hapo ni mbaya sana, badala yakufunga milango, basi utakuta kila pahali pameachwa milango na madirisha ile siri haipatikani. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, atakapokuja anieleze jengo hili limefikia wapi katika ukamilishaji wake.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, wameonesha katika kitabu hiki kwamba kuna hatua ya kutafuta mkandarasi mpya wa ujenzi wa ofisi Pemba. Kwanza

nimpongeze sana na niipongeze Wizara ya Fedha kwamba hii ilikuwa na mimi ni maoni yangu katika ofisi za Pemba, kuona kila siku zinakodi majengo binafsi na wengine wamo katika majengo mabovu, niipongeze sana serikali kwa kuliona hili na kuona kwamba tayari hatua zimeanza kuchukuliwa.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki ameeleza kwamba wizara ina majukumu ya kusimamia fedha za umma na wahasibu. Namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha katika kazi zake za kusimamia masuala haya kwanza mfumo wa watendaji nao ubadilike, kama vile washika fedha. Washika fedha sasa imekuwa wao wanamilikisha ofisi. Mtu anaweza kufika miaka 20 ni mshika fedha wa taasisi moja, suala hili naona ni tatizo. Kama vile wanavyohamishwa wahasibu basi na hawa naomba sana nao wabadilishwe huku na huku, itawasaidia katika kujenga uwezo na ufahamu wa mambo mbali mbali kwa kupitia kila taasisi na muundo wake.

Mhe. Mwenyekiti, pia, suala zima la mafunzo ya wahasibu, ndani ya kitabu hiki imeonesha mafunzo ya wahasibu na wakaguzi wa ndani. Mimi nilitaka kujua katika ukaguzi huu wa wahasibu je, mafunzo haya yamefika Pemba na wamefanya kwa wahasibu na wakaguzi wangapi. Je, utaratibu huo wa mafunzo unaotolewa unafanywa kwa vipimo vyake au tunapitisha tu, kwa sababu lengo la mafunzo ni kuweza kufanya kazi kitaaluma, sio kwa mazowea. Sasa je, kuna vipimo gani ambavyo wanavitumia katika kuona kwamba mafunzo yetu yameleta tija, naomba sana suala hili ushauri wangu huo uangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kuna masuala ya mishahara, masuala haya nimebaini kwamba kuna tofauti, mishahara ya wafanyakazi wa serikalini na mishahara ya wafanyakazi wa mashirika ya umma, kwa nini iwe tofauti na sote tunajenga nyumba moja. Leo ukimpata mfanyakazi anayefanyakazi katika Shirika pengine la Bima au Shirika la Umme, basi anakuwa ni tofauti. Mfanyakazi yule yule hata kama ni mfyagiaji, basi ukiambiwa yuko Shirika la Bima, Shirika la Umeme au pengine *TRA* au wanapishana mishahara tofauti na ofisi nyengine, kwa nini sote tunajenga nyumba moja, kwa hivyo, tusipishane katika nafasi ambazo kuwa ni moja. Mfyagiaji awe ni sawa sawa na ofisi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije katika suala zima la Chuo cha Chwaka. Mhe. Mwenyekiti, chuo hiki tushukuru sana kwa kuwepo hapa Zanzibar, hali ambayo ilikuwa ikitulazimu gharama kubwa sana kwenda kuipata huduma kama hizi Tanzania Bara au na kwengineko, leo kiko hapa kimechukua jukumu la kufahamisha na kuwaelimisha wananchi wetu na vijana wetu ambao wanatoka mashuleni. Lakini naona kwamba watu hawa baada ya

kumaliza wengi wamebaki mitaani na sisi tunawahitaji. Kwa hivyo, naiomba sana serikali tuangalie ile elimu iliyopo kule isibaki mitaani iweze kuja serikalini kufanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu za Serikali inahitaji wataalamu wakaguzi, kwa nini hatuwachukuwi watu hawa, ambapo tutakuwa tunatengeneza ajira, lakini tunapata watu ambao bado hawajaanza kupata zile cheche za maofisi, kuliko kubadilishana kwenda huku na huku, watu wale wataweza kusaidia sana, watakapofika katika ofisi hii watapewa mafunzo watakuwa ni wapya kabisa na wao wataweza kufanyakazi za ukaguzi bila ya kufanya ubadhirifu wowote, hawataona kitu gani ambacho wenzao waliopita wanafanya, kwa vile wao watakuwa ni wapya wataendelea na mfumo ambao watakuwa wanaelekezwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima la mfumo wa *ZSSF*. Huu ni mfuko ambao ulianzishwa mwaka 1998 kwa malengo ya kumsaidia mfanyakazi. Malengo ni mazuri naipongeza sana serikali kwa kuanzisha mfuko huu Zanzibar. Lakini kila zuri haliwachi kuwa na kasoro. Kumekuwa na kasoro ambazo tunazipigia kelele sana, mfanyakazi ambaye ameachishwa kazi au ameacha kazi kwa hiyari yake, kwa nini mfanyakazi kama huyu kama anadai kile chake keshaamua hana kazi tena nyengine ya serikali atakayoifanya, hafanyiwi ili aweze kupatiwa mafao yake. Kwa sababu ukimwambia mpaka afike miaka 60 au 55 hujui kama atafika. Lakini mtu huyu leo keshaacha kazi anataka chake ili aweze kujiandaa na maisha mengine inakuwa ni kero, tena ni kero kubwa sana.

Kwa hivyo, tunaomba sana huu mfuko hii sheria iwaangalie tena. Walisema wakati wa kuingia ukishachangia miezi 60 utaweza kupata mafao, leo inabadilika. Hebu tuwaeleze wafanyakazi walistaafu au kuacha kazi na waliokuwa hawajaacha kazi wajijuwe mbele wanavyokwenda.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la michango ya taasisi zetu ambazo ni za serikali zinakusanya mapato. Huu utaratibu wa kutumia hii *electronic* naona ni vyema sana tukaufanyia haraka ili ukaanza kufanyakazi mara moja, kwa sababu mapato yanapotea. Mhe. Spika, unakwenda katika taasisi au wahudumu mbali mbali unatoa fedha lakini hupati risiti, ni kwa macho yangu mwenyewe nimeona hili likitendeka, hata hapa watu wa Baraza la Mji unafika pale unaingia na gari pale, wakikutizama kidogo kama una koti basi watakupa risiti au suti basi wataogopa, lakini nimeona hivi kwa macho yangu watu wanalipa fedha hawapewi risiti hiyo tayari imekwenda hiyo. Kwa

hivyo, kama tunataka kufanyakazi kweli basi tuandae vyombo hivi ambavyo vitaweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, niende tena kwenye Shirika la Bima. Nimeona katika kitabu hiki kuna shilingi milioni 936 za maendeleo. Naomba nifahamishwe na lifahamishwe Baraza hili, hivi Shirika la Bima linafanya maendeleo gani kwa fedha hizi, zinakwenda wapi, huu mchango wangu naomba nipate maelekezo ili na mimi niweze kujua, kama Shirika la Bima linafanyakazi za maendeleo ni yapi hata zikawekwa fedha kama hizi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki cha hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ameonesha vipaumbele vya wizara, kusimamia upatikanaji wa mapato bilioni 824, ni sawa, lakini kazi hii tutaifanya kwa pamoja *Inshaallah*, kwa kushirikiana yeye na sisi tutahakikisha fedha hii inapatikana ili yale malengo yaliyopangwa yaweze kufikiwa.

Lakini kuna suala la kipaumbele cha ulipaji wa madeni. Madeni yapo mengi na yote yameelekezwa upande wa Wizara ya Fedha kwa sababu yeye ndiye mlipaji. Kuna madeni ya wastaafu imekuwa ni kero. Huko nyuma tuliambiwa tayari mfuko umeshakua mzuri kwamba ukimaliza kustaafu unakaa mwezi mmoja unapata fedha zao, sasa hivi kuna watu zaidi ya miezi sita hawajapata mafao yao. Hapa tunapoelekea kuna watu wanataka kwenda kuhijji, fedha hizo zimekwama. Kama kuna wafanyakazi wamejipangia kwamba mimi niende katika kutekeleza ibada hii ya Hijja katika fungu hili, leo imekuwa ni kero, unamnyima fursa hii mauti yakimfika sijui itakuwaje na yeye chake kipo hajaweza kukipata.

Naomba sana wanapotokeze wafanyakazi waliostaafu kama wameleta maombi haya ya kutaka kwenda Hijja basi wapewe kipaumbele, hasa hivi sasa tupo kwenye mwezi wa Ramadhani, harakati zimeanza na Mhe. Waziri wa Fedha suala hili ulipe kipaumbele na yeye Mwenyezi Mungu atamsaidia sana katika shughuli zake za kazi.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la jengo la Wizara ya Fedha na Mipango liliopo Pemba, jirani na Mfuko wa *ZSSF*. Jengo hili kila mmoja analipigia kelele, na mimi pia linaniuma sana, kuona fedha ya serikali pale imepotea, imekuwa ni gofu pale na hatujui kinachoendelea. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja aniambie je, ni hatua gani ambazo mpaka sasa zimechukuliwa, ama mkandarasi yule ni hatua gani ambazo amechukuliwa, na jengo lile litabaki pale kuwa gofu hadi lini, kwa sababu ni tatizo na ni hasara kwa lile Jengo la Mfuko wa *ZSSF* pale. Jengo lile

likiporomoka hujui atakuwemo nani pale, viongozi mbali mbali wanafika pale wa nchi hii wanakuwepo mule katika hoteli ile. Huwezi kujua ni saa ngapi litaporomoka. Kwa hivyo, naomba kama limeshindikana jengo lile liondolewe mara moja, pabakie kiwanja tuangalie nini tutafanya. Hili ni ombi langu kwa Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba mchango wangu niishie hapa. Baada ya hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia juu ya mia bila ya matatizo yoyote. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Shehe Hamad Mattar. Anafuata Mhe. Said Omar Said, Mhe. Miraji Khamis Mussa na ajitayarishe Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu *Jalla Subhanahu Wataallah*, kwa kuniwezesha asubuhi hii kuwepo katika *Majlis* tukufu hii. Nikushukuru wewe kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nimpongeze sana Mhe. Waziri, kutokana na haya yaliomo humu katika kitabu hiki, ambacho kinaelekeza mafanikio ya haja za wananchi wa Zanzibar. Vile vile, nimshukuru tena au nimpongeze tena Mhe. Waziri, kwa jinsi alivyoiwasilisha hii hotuba kwa umahiri mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika, niwapongeze na wasaidizi wake wote waliomsaidia kumrahisishia kazi hii na ikawa nyepesi kuiwasilisha kwake. Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu hautakuwa mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze utangulizi wangu kwa kumkumbusha tu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, hasa ilivyokuwa leo ni siku tukufu ya Ijumaa. Sikubahatika tu kuvaa kanzu, lakini leo ilikuwa niwe na kanzu. Napenda sana nimkumbushe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, najua kwamba yeye anajua na siku zote anayekumbushwa ni yule anayejua ndiye anayekumbushwa.

Kwa mfano, Qurani inaitwa dhikri, kwa sababu gani, kwa sababu ni ukumbusho. Sasa haya tunayosomewa, wanasema hao wataalamu kwamba haya tunayaelewa sisi. Kwa hivyo, kutokana na *back ground* tunakotoka tunaelewa kila kitu. Sasa huu umekuja kama ni ukumbusho tu, kila mmoja anaelewa. Huyu mwizi, huyu ni mtekelezaji, kila mmoja anaelewa hivyo, lakini sasa umekuja huu ni ukumbusho. Kwa kweli hii Ijumaa kidogo nitaje, amesema Mwenyezi Mungu (Surat Al Qiyama 75:14 - 15) *Balil-insanu* a*'laa nafsihi baswirah*, yaani huyu mwanadamu yeye ndani ya nafsi yake anaona, kuwa huu

niufanyao ni ubadhirifu, huu niufanyao ni wizi kwa mfano, huu niufanyao ni uzembe, anaelewa mwenyewe, *walau alkaamaadhira*, japo akajitia nyuzuru, kama mimi sifahamu, sijui baya wala jema. Sasa kama hujui baya mbona ukifanya unajificha, kama hujui baya ungefanya hadharani, lakini ni kwamba unajua.

Kwa hivyo, mimi ningependa nichukuwe nafasi hii kama utangulizi kwa kumkumbusha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwamba yeye ndio *referee* humu, na sisi tuliobakia ni wapeperusha vibendera, yaani *linesman*, kazi yetu ni kuangalia nani anayekwenda faulu tukapeperusha kibendera, nani aliyekuwa *outside* tukapeperusha kibendera kwake yeye. Sasa mwenyewe ataamua kukuangalia au kukufumbia macho, lakini sisi ni lazima tupeperushe vibendera kwa sababu tumewekwa kama ni ma-*linesmen* kumsaidia yeye kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe, wengi tumeomba sana katika huko tulikopita, na hiki kitabu kimewekwa hapa mwisho kutokana na umuhimu wake. Kama Qurani, Qurani imewekwa mwisho, yaani inarekebisha vitabu vilivyopita. Kwa hivyo, na hiki kimewekwa mwisho ili kusahihisha maombi yetu yaliyopita. Hapa napenda sana kumkumbusha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, tulimuomba sisi, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwamba, awapatie posho walimu wa Vyuo vya Qurani. Sasa kama yeye yuko tayari basi anangoja kauli yako wewe, yeye hawezi akafanya hivyo kama hujamuwezesha. Napenda kukukumbusha tu kwamba hao tuliowaombea wale walimu wa vyuo, vyuo 52 ambavyo vilisajiliwa basi mwezeshaji ni wewe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika hotuba. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi wanailalamikia serikali yao kutokana na ukubwa wake. Maana yake serikali kutokana na ukubwa wake, halafu mambo mengi imechukua na serikali yenyewe ni ndogo. Uchumi ni mdogo, lakini utakuta pamoja na kwamba kulikuwa na wizara kumi na sita zikapunguzwa zikafikia kumi na tatu, lakini hakuna aliyeondoshwa, hakuna mtu yeyote aliyepunguzwa mzigo upo pale pale, sasa wao wananchi wana wasi wasi. Je, yale yaliyoelezwa humu yatawafikia. Hapo ningemuomba Mhe. Waziri, awaeleze hao wananchi yatawafikia kwa moja, mbili, tatu.

Kifungu cha 13, *ZRB* na *TRA*, mimi nipongeze sana taasisi hizi kwa kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana na ujasiri mkubwa wa kukusanya fedha nyingi, fedha hazikusanywi kwa upole upole, fedha zinakusanywa kwa ukakamavu wa hali ya juu, kwa hivyo, niwapongeze sana kwa kuweza kukusanya fedha ambazo zitatusaidia katika maendeleo yetu.

Lakini Mhe. Waziri, hapo hakuja changamoto na mimi naamini kwamba zipo changamoto, moja alitangulia mwenzangu kwamba wafanyakazi hawakuangalia makadirio halisi, alisema mmoja katoa ufafanuzi inatosha, lakini jengine bado wako wakusanyaji wanaochota fedha kwa ajili ya faida zao hawa tutawafuata. Sisi tulivyoingia humu tulikamata msahafu na msahafu hauna mchezo ule, tulisema tutatekeleza haja za wananchi waliotuleta hapa, kwa hivyo, tutatekeleza.

Kifungu cha 43, ukurasa wa 24, *ZIPA* Mhe. Mwenyekiti, mimi yamenifurahisha sana maelezo ya Mhe. Waziri kwamba, ametenga fedha kwa ajili ya kuendeleza uwekezaji Fumba na Micheweni, tumeanza kuona ishara njema za maelezo haya kwamba Fumba tayari ameshapelekwa muwekezaji na tayari ameshaanza kuchukua hatua zake, lakini Micheweni bado. Tunamuomba Mhe. Waziri, atuelekeze na sisi katika Wilaya ya Micheweni, Micheweni kuna eneo kubwa, watu hawalimi katika maeneo hayo, watu hawachungi ng'ombe, lipo tu limekaa kwa ajili ya uwekezaji, kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri, atuelekeze na sisi kule Micheweni na sisi tunaloliomba tunaomba Muwekezaji wa sekta ya viwanda, wenzangu wameshaanza kuzungumza, sisi kwetu tunaomba uwekezaji wa sekta za viwanda, sisi nyumba tutajenga wenyewe. Sisi tunataka sekta za viwanda ili watu wetu wapate ajira kule baadae kila mmoja atajenga nyumba anayotaka mwenyewe.

Kifungu cha 45, ukurasa wa 25, Mfuko wa Hifadhi. Mhe. Mwenyekiti, niupongeze sana mfuko huu wa hifadhi ambao unawasaidia wale wastaafu kuweza kupata malipo yao bila ya matatizo yoyote pamoja na malipo ya uzeeni, lakini tukumbuke kitu kimoja tukumbuke sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuna wafanyakazi waliotutangulia sisi wa nyuma hawa tuangalie sana kwa jicho la huruma na imani. Wafanyakazi hawa ambao walistaafu siku za nyuma pencheni yao labda ni shilingi 40,000, sasa jamaa hiyo mwenzi mzima mfanyakazi ameifanyia kazi Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa muda huo uliotajwa na sheria, kama miaka hamsini au sitini, leo analipwa pencheni Shs. 40,000 zimsaidie nini, Shs. 40,000 hazinunui hata polo. Maana yake angalau ingekuwa Shs. 55,000 ambayo ndio bei ya polo ingekuwa angalau nafuu, lakini Shs. 40,000 anapata nini.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, awaangalie wale waliostaafu wakati huo ambayo ilikuwa mapato yao ile mishahara yenyewe ilikuwa iko chini, ambayo imesababisha mpaka pencheni zao zimekuwa chini, tunawaomba sana na pia nawaomba Waheshimiwa, wenzangu kwamba hao ndio waliotufundisha sisi mpaka sisi tukawawemo humu, kwa hivyo, lazima tuungane ili kuwatetea tuwe pamoja, tuseme *we are full together*.

Kifungu cha 45, ukurasa wa 26, Benki ya Watu wa Zanzibar, mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Wingwi niwapongeze sana Benki ya Watu wa Zanzibar kuweza kurejesha huduma za kibenki katika Makao Mkuu ya Wilaya zetu, muda mrefu hususani kule Pemba sijui huku, lakini kule muda mrefu ilikuwa Benki inayotumiwa ni benki moja tu ya Chake Chake, mtu kutoka Makangale kuja Chake Chake kwa kweli ni kero kubwa. Mtu kutoka Kiuyu Maziwa Ng'ombe ambae atalazimika aende Chake Chake ni kero kubwa, lakini ulifikia wakati Wizara ikaamua kuzirejesha huduma zile katika Wilaya. Sasa kwa upande wa Pemba huduma zinapatikana katika Wilaya ya Mkoani na Wilaya ya Wete, bado Wilaya yetu ya Micheweni tunamuomba sana Mhe. Waziri, atuwekee na sisi huduma katika Makao Makuu yetu ya Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, tuelewe kwamba kama kutatolewa zawadi kwa Wilaya masikini ni Micheweni tutapata zawadi sisi, hiyo ndio nyimbo tu inaeleweka Mhe. Waziri, anaielewa hiyo na pia anaelewa kwamba watu hukutana pale kwenye pesa ndipo wanapokutana, sasa angelituwekea kituo kule watu wangelikusanyika kule, wakikusanyika watu ndio panapokuja maendeleo, tunamuomba sana Mhe. Waziri na sisi atupe kipaumbele ili na sisi tuweze kufaidika kwa huduma za kijamii.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, una dakika mbili.

Mhe. Said Omar Said: Zinanitosha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kutokana na dosari zilizopo katika utoaji wa fedha katika Benki zetu za Pemba hususan Chake Chake kwa sababu ndio benki kuu pale, Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli pana utaratibu mbaya sana pale. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri, irekebishwe ile hali, wewe unakwenda kuchukua fedha pale unazungurukwa na macho mia nne, unakwenda kuchukua fedha nyingi wanakupa pale pale. Mimi nasema *with confidence,* nimekwenda mimi kuchukua milioni thamanini Chake Chake pale pesa za *SACCOS* kwa sababu katika Idara ya Elimu Pemba tunayo *SACCOS* ndani ya Wizara yetu nilikokuweko wakati mimi nilikuwa Mwenyekiti wa hiyo *SACCOS* inaitwa JITAMBUE *SACCOS* mpaka leo bado sijajiuzulu, lakini nimetoka kwa kuja huku.

Kwa hivyo, nikaenda mimi nikapelekwa *Bank* kule walimu tayari wameshapiga msongo pale wamekuja kuchukua mikopo yao pale, ikalazimika mimi kwenda benki kufika kule nikaenda ku-*draw* milioni 80, aaa, mimi mwenyewe nimemshangaa yule mhudumu badala ya kuniambia njoo sehemu fulani au

nenda chumba fulani kama hapa Zanzibar mimi nimpongeze sana Meneja wa *PBZ* Unguja nzuri sana. Baada ya kuona hali ile ananihisabia milioni 80 juu ya macho mia nne nikapiga simu Wizarani kule nikaletewa gari. Je, ningelizichukuwa vile, watu mia nne wapo nyuma wananiangalia, ingelikuwaje mimi, ndio baadae tukaanzisha utaratibu mwengine wa kutumia *check* ambao wakija wahusika ambao ni walimu au wafanyakazi wa Wizara ya Elimu wanakwenda wenyewe kutokana na dosari hiyo tuliyoikuta siku hiyo. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri, irekebishe hali ile.

Namalizia, niipongeze sana Wizara hii kwa kufanya uhakiki wa kila kipindi ili kutafuta wafanyakazi hewa, hapa naomba nimuulize Waziri kwamba kabla ya mwaka 2016 hicho kipindi cha mwisho Mhe. Waziri, alivyokwenda kufanya uhakiki kule watendaji wake, ni watu wangapi waliogunduliwa ni wafanyakazi hewa.

Mwisho kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wingwi tunaiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.(*Makofi*)

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu na watendaji wake kwa uwasilishaji mzuri na maandalizi mazuri wa kitabu hichi kilichotosheleza mahitaji ya Wazanzibari katika kuwatumikia, niwapongeze sana kwa hotuba yao hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nitatumia muda wangu kwa makini sana ili nisije nikazidisha dakika, pengine wizi wa dakika pia unaweza ukapungua, naomba nielekeze moja kwa moja mchango wangu kwenye bodi ya mapato *ZRB*. Kwanza niwapongeze wafanyakazi wa bodi hii ya mapato kwa kusimamia vizuri mapato ya Serikali. Lakini sambamba na hilo, nilitaka kujua kuna eneo moja la uhaulishaji kwa umiliki wa mahoteli, utaratibu ambao unatumika najua upo, lakini nijue tu kwa mwaka wa fedha 2014 mpaka kufikia sasa 2016 ni mahotali mangapi waliobadilisha umiliki na kiasi gani cha fedha kimepatikana. Kwa sababu unajua kwenye eneo hili kuna fedha nyingi sana zinatakiwa zilipwe kwa mujibu wa ile *transaction* inayofanyika kutoka mmiliki mmoja kwenda kwa mmiliki mwengine. Lakini kama kuna changamoto gani tunazozipata katika eneo hili basi naomba Mhe. Waziri, atakapokuja atupe ili tuweze kumsaidia kudhibiti mapato ya eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, niende sasa kwenye kodi zinazotokana na *ATM* na nyumba hizi zinazokodishwa za wamiliki binafsi, tumeona ziko *Bank* zina *ATM*

Machine zinamilikiwa na watu binafsi wanakodisha hizi nafasi za kuweka *ATM* kama benki, lakini wanakodisha nyumba zao kwa kuweka benki hapa ipo kodi, sitaki ile kodi ya ujumla kwa kuwepo kwa benki wanachangia kiasi gani, nataka yule mmliki wa lile jengo aliyekodisha *ATM Machine* na aliyekodisha nyumba. Kwa sababu zipo nyumba nyingi tunaziona wamiliki hawa wameingia mikataba na Benki mbali mbali, kwa hivyo, hapa pana kodi zetu, kwa hivyo, nataka kujua kiasi gani katika mwaka wa fedha huu tumepata kodi yetu kupitia umiliki huo na ukodishwaji huo wa benki kutoka mmiliki binafsi kwenda katika benki, huyu mmiliki binafsi huyu ndio anatakiwa ile kodi yake achangie Serikali, nilikuwa nataka kujua kiasi gani cha fedha kimetumika katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nihame hapo sasa nihamie Wizara ya Fedha kwenye utaratibu wa kuwachangia sehemu ya *Tuition Fee* wanafunzi wanaosoma *Diploma* na *Degree* katika chuo cha *Zanzibar University* (*ZU)*, hapa Mhe. Waziri, yapo malalamiko makubwa ambayo ni dhana nzuri ya kuwasomesha vijana wetu, lakini hawapati pesa kwa wakati wanazuiwa mitihani yao na wako wanafunzi Jumatatu ijayo wanaingia kwenye mitihani, utaratibu gani ambao tutawasaidia kwa kipindi hichi ili waweze kufanya mitihani yao, lakini hata wakifanya hawa baadae pia fedha zinachelewa hizo za mchango tu katika *Tuition Fee*. Nasema ni dhana nzuri, wazo zuri na niwapongeze Wizara kwa hatua hiyo ya kuwasaidia vijana hawa kuengeza elimu zao, lakini wanafika pahala wanamaliza wanazuiliwa vyeti vyao hata zile *transcripts* ambazo ni sehemu ya tegemeo lao la kuomba hizo ajira zenyewe. Kwa hivyo, ni lini Serikali kupitia Wizara yako itawasaidia wanafunzi hawa na tukizingatia Jumatatu tu keshokutwa wanafanya mitihani yao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekeze mchangio wangu katika Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, niwapongeze sana walimu na viongozi wanaoendesha Chuo hichi, wamefanya kazi nzuri sana, jitihada yao imeonekana tumepata vijana wazuri wanaoweza kufanya kazi vizuri katika kulitumikia taifa lao katika sekta ya fedha. Lakini niombe sana Serikali kwa sababu upo mnong'ono wa kuunganisha vyuo hivi kwenye kuviunganisha na *SUZA*, ni wazo zuri lakini wakati fulani unapounganisha vitu vingi katika Chuo kimoja cha *SUZA* unaweza ukapoteza hata ule ufanisi wa kudhibiti yale mafunzo yenyewe.

Sasa ningeomba Serikali hapa kwa sababu Chuo cha Uongozi wa Fedha kinafanya kazi vizuri kwenye eneo hili basi bora tuishauri *SUZA* ianzishe *Faculty* inayofanana na zile kozi ambazo zinatolewa huku Chuo cha Uongozi wa Fedha ili pawe pana ushindani mzuri katika vyuo hivi viwili, kuliko kwenda kuiunganisha. Kwa hivyo, naiomba sana Serikali kwenye jambo hili izingatie

sana juhudi katika Chuo hichi zinafanyika na tunaona matokeo yake wanafanyakazi vizuri. Kwa hivyo, niwaombe tu serikali kama kuna dhana ile ya kuviunganisha vyuo hivi kwa chuo hiki watubakishie, lakini waishauri *SUZA* ianzishe *Faculty* ili tutoe ushindani wa kimasomo katika vyuo hivi viwili.

Lakini pia hapo hapo niwaombe sana viongozi wa chuo wapo walimu wanafanya kazi kwa muda wa ziada kuliko ule muda ambao umewekwa kisheria. Basi niwaombee tu viongozi hawa kwa kazi nzuri waliokwisha kuifanya basi wawapatie alau *overtime* na wao wawe na moyo mzuri wa kufanya kazi katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nende sasa katika eneo la miradi ya maendeleo, wamezungumza wenzangu na mimi naomba nielekeze nguvu zangu katika eneo hili la miradi ya maendeleo. Mimi niipongeze wizara kama nilivyoipongeza mwanzo wanafanya kazi kubwa sana ya ku-*plan* kutengeneza utaratibu wa kutafuta fedha, lakini pia kutengeneza utaratibu wa kutafuta wafadhili katika kusimamia miradi yetu ya maendeleo.

Niwapongeze tena Wizara ya Fedha zimetafutwa fedha za *ZUSP* wamezisimamia na zinakwenda vizuri na miradi hii inaonekana matokeo yake, nawapongeza sana. Lakini yako maeneo tunawaamini wenzetu baadae wanatufelisha, dhima kubwa hii inakuja kubakia Wizara ya Fedha. Mimi niende katika fedha ambazo tulizielekeza kwenye miradi ya majengo ya Wizara ya Elimu, ni dhana nzuri, Wizara ya Elimu wamejenga majengo tukenda tukayakagua sasa hivi utakuta majengo yale hayako katika kiwango. Majengo yamejengwa miaka miwili haijafika basi sasa hivi yanavuja, lakini yameanza nyufa yote. Maana angalau unajenga majengo kumi ukute matatu tu yana kiwango kizuri, lakini yameanza nyufa yote, pia, yanavuja sehemu kubwa, yaani asilimia 90 ya huo ujenzi wa majengo yanavuja, maana kama umejenga kumi basi manane yanavuja, sasa huyu mkandarasi gani.

Sasa niiombe Wizara ya Fedha, kwa sababu katika mpango ambao upo sasa tuna skuli kumi na moja ambazo tunataka kuzijenga katika mwaka wa fedha huu; ziko skuli kumi za sekondari laki moja ya msingi, wasimamie wenyewe utaratibu wa kuwapata wajenzi wa skuli hizi. Vyenginevyo, tutakuja kurudi miaka mitatu hapa tunapitisha fungu la ukarabati wa skuli hazijafika miaka mitatu. Kwa hivyo, niiombe sana Wizara ya Fedha katika maeneo haya muhimu ya ukamilishaji wa miradi ya maendeleo, wenzangu wamelalamika barabara unajiuliza wakati mwengine hatuna wakandarasi wazuri wa kusimamia utaratibu wa kuwapata wakandarasi hawa, lipo tatizo katika

ukamilishaji wa miradi ya maendeleo. Lakini dhana nzuri ninawapongeza wizara lakini wasimamie kuwapata wajenzi watakaosimamia miradi ya maendeleo, mimi kwangu hususan hii miradi ya ujenzi wa skuli za Wizara ya Elimu. Kwa hivyo, ninamuomba waziri alizingatie hilo, lakini pia wenzangu wamezungumza masuala ya Kanuni ya 120(2). Kama Kamati Teule itaundwa basi pia waliingize suala hili la majengo la Wizara ya Elimu, kuna kadhia kubwa sana, alau tuje tuishauri Serikali nini cha kufanya.

Pia, wasiingize *AGAPE* tu, waingize hata suala la Uwanja wa Gombani kwa sababu hizi ni pesa za miradi. Tumetafuta wajenzi wamejenga tatan, lakini matokeo yake hamna kitu, fedha imeliwa, ujenzi ule wameharibu, tunaambiwa tu serikali inachukua hatua zake kweli, lakini nasema ili tujuwe uhalisia katika ujenzi wa tatan ile basi itakapoundwa Kamati Teule ukiacha yale waliotaja wenzangu liingizwe hili la ujenzi wa tatan, liingizwe suala la miradi hii ya maendeleo ya Wizara ya Elimu kwa skuli zilizojengwa hivi karibuni tuone serikali tunakuja kuishauri vipi.

Lakini suala jengine la majukumu la wizara hii, Mhe. Mwenyekiti, juzi tu nilizungumzia mimi suala la Bodi ya Wakandarasi, bodi ile sehemu kubwa maana pale kuwa wahasibu ambao wahasibu ni mali ya Wizara ya Fedha. Wakati huo huo kunako Taasisi kuna ma-*internal auditors* ni mali ya Wizara ya Fedha, watendaji wetu hawa wanapokwenda katika taasisi kama hizi kuzifanyia kazi lazima waoneshe uwezo wa kuisaidia serikali. Mimi juzi nimetaka kujua kiasi gani cha fedha kimepatikana, maana fedha zile ndio mchango mkubwa wa uendeshaji wa serikali hii, sio kila eneo tunaitegemea Wizara ya Fedha ikusanye kwengine wakatumie watu katika Taasisi za Serikali, lakini na Taasisi zenyewe ziwe na uwezo wa kukusanya fedha. Kwa hivyo, eneo hili lina jibu, ninaiomba pia tutapofikia hatua ya Kamati Teule ile na hapa ipitie pana fedha nyingi sana za serikali zinapotea hapa kinyume na utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niende katika mapato, katika kitabu kuna mapato yanayotokana na vifaa chakavu. Naomba Mhe. Waziri, utakapokuja kwa sababu mimi hapa moja ya wasiwasi wangu vifaa chakavu hivi utaratibu wake tunaupeleka kwenye *asset register*. Hizi *asset register* hata katika mawizara na mashirika ya serikali hamna, sasa utaratibu gani ambao mpaka unatupeleka kwenye *disposal* hii ya kuuza vifaa chakavu unaotumika.

Haraka haraka dakika yangu moja. Katika kitabu pia kuna kodi ya mashamba ya mipira. 2015/2016 yapo makadirio, lakini 2016/2017 makadirio hapana, ni sababu gani zilizopelekea kodi ile ya mashamba ya mipira kuwa imekosekana.

Mhe. Mwenyekiti, mengine nitachangia kwa maandishi, nisije nikaiba muda nikafungua.

Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 90, asilimia 10 ninakuja kumrejeshea waziri baada ya ufafanuzi wa masuala haya. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilimsikia waziri dhamana wa Vikosi vya SMZ Mhe. Haji Omar Kheri, akisema Jeshi la Polisi ndio litatoa kauli kuhusu habari ya vifo vilivyotokea.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, kuhusu utaratibu kifungu gani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni ya 63, kinasema;

"Mjumbe anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu, lakini mjumbe anapofanya hivi itabidi ataje kanuni ya Baraza iliyokiukwa".

Mhe. Mwenyekiti, umemsikia Mhe. Haji Omar Kheri, akisema kuwa Jeshi la Polisi ndio litakalotoa utaratibu wa habari kama kuna mtu kafa au hakufa. Lakini uzoefu serikali ndio inayotoa maelezo, tumeshuhudia meli ya *Spice Islander* kuzama, serikali ikatoa kauli ya mauti ya vifo vile, *M.V Sky Gate,* serikali ikatoa kauli, Kilimanjaro ikatoa kauli. Mawaziri ndio wanaowajibika humu kujibu masuala, wala asifikirie waziri sisi kama tunampiga *fine* humu au tutamuhuku. Hatuwezi kumpiga *fine* waziri sisi, lakini mawaziri ndio wanaowajibika katika Baraza. Polisi kazi yake kukamata na kuchunguza.

Mimi nilikuwa nataka serikali itoe kauli kama ipo sawa na kama haipo basi. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati kabisa na nataka nijitahidi nimpe Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, angalau dakika 5. Mimi kabla sijaanza kuchangia lolote kwanza naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri, kwa asilimia mia moja. Na sababu za kusema hivyo mimi ni mdau wa Kamati na nilichangia kwenye Kamati yangu mambo mengi nikatoa mawazo yangu na fikra, lakini unajua mambo huwa hayatoshi na kila siku yanaongezeka.

Nataka nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Katibu wake Mkuu, kubwa ambalo nataka kumwambia Mhe. Waziri kwamba amepata dhamana kubwa sana na hili eneo gumu, sote tunaelewa yeye Waziri na Katibu Mkuu wake ni watu ambao wana uwezo mkubwa na upeo, ni watu wa waadilifu lakini nataka niwasaidie kuwapa indhari kwamba wapo katika eneo lenye mapapa na manyangumi katika masuala makubwa ya ufisadi wa nchi hii. Sasa sifa zao zisije zikapotea kutokana na waliowazunguka.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kutoa msisitizo tu kumuomba Mhe. Waziri, kujitahidi kufanya uharakishaji wa kufanya mabadiliko kwa sababu limo ndani ya utaratibu wa sheria yao katika watu wa kada ya uhasibu kuona wanahamishwa haraka kwa sababu wamedumu katika vipindi virefu pasipo kubadilishwa. Nilizungumza katika vikao vilivyopita Mhe. Waziri, anatoa ahadi ya kwamba tutabadilisha haraka lakini tukimaliza bado ile hali inabaki kuendelea kila siku, wenzangu wamechangia na mimi ninasisitiza.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie katika suala la *ZRB*, kila mtu amechangia kwa namna yake, nataka nimsaidie Mhe. Waziri, kwamba hiki kitengo kina matatizo makubwa sana katika kutoa taarifa za ukweli kwa ukusanyaji wa kodi na hususan katika maeneo ya mahoteli na wafanyabiashara. Maafisa wake wanapofika katika maeneo na kuona taarifa sahihi na kuwataka watu waje walipe kipindi cha kurudi katika taasisi zao wao ndio wanaotumia muda ukiwapigia simu wale wafanyabiashara au wafanyabiashara huwapigia wale maafisa kwamba kodi yangu kubwa nataka tuje tukae tuzungumze. Matokeo yake kama mfanyabiashara anatakiwa alipe kodi ya milioni ishirini basi panafanyika mazungumzo ya kukatisha kodi ile atalipa milioni tano kilichobakia mtu anapewa pesa mkononi. Sasa haya ni matatizo ambayo yanapelekea kuikosesha pesa serikali yetu kama baadhi ya watendaji wa *ZRB* kutokuwa waaminifu.

Chengine ninamuomba Mhe. Waziri, aangalie sana kitengo cha *procurement* pamoja na watu wa *tender board*, sheria zipo, baadhi ya wenzangu wamejaribu kutaja mapungufu na wametaka tuje kurekebisha sheria. Lakini pamoja na mapungufu yaliyokuwepo, lakini pia tuna mapungufu ya baadhi ya maofisa kutokuwa waaminifu na kutumia vibaya vitengo hivi.

Chengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka Mhe. Waziri, atusaidie au atueleze mipango ya serikali ya wizara yake katika suala zima la kutumia *electronic machine*. Jitihada najua za serikali zimeanza lakini nalo hili nataka nimueleze pia lilianza tangu waziri aliyepita mpaka akafika kutoa muda wa kuanza kwa zoezi hili. Sasa nasema pasipo na kuanza kwa utaratibu wa

electronic bado tutakuwa tunalalamika kila siku kwa suala la *manual*, wafanyakazi wengi si waaminifu na wanapotumia *manual* hadaa zinakuwa zinatumika na zinaweza kusababisha mapato kuvuja katika taasisi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba Mhe. Waziri, atusaidie katika suala zima la kuwasomesha vijana wetu. Mhe. Miraji, yeye alilalamika kwamba ucheleweshaji wa fedha kuingiziwa vijana ambao wako vyuoni, mimi niko tofauti na yeye kidogo tu. Mimi ninachotaka kumuomba Mhe. Waziri, kwa kuwa serikali kwa nia njema kabisa ilianzisha chombo cha Bodi wa Mfuko wa Elimu ya Juu kuwakopesa vijana fedha kwa ajili ya kujipatia elimu. Ninamuomba Mhe. Waziri, aangalie kwa kina bado kuna utamaduni wa baadhi ya mawizara kuomba fedha na kuingiziwa kuwasomesha wafanyakazi wao. Hata katika bajeti ya Wizara ya Kilimo ya safari hilo tuliliona na tulilipigia kelele sana, wana *more than billion* ambazo wametenga kuwasomesha vijana wao, nasema serikali ina nia njema na ndio maana wakaanzisha chombo maalum ili kutoa mikopo kuwasomesha vijana, athari ya kupeleka pesa mawizarani Mhe. Waziri, nataka nikusaidie, kwamba ukiingiza pesa kwenye mawizara, maana yake anayesomeshwa hana kipengele cha kurejesha fedha serikalini.

Maana yake kwamba serikali itakuwa inatoa pesa lakini baada ya muda tutawakosesha baadhi ya vijana kutokupata fursa ya kusoma kwa sababu uwezo wa serikali utakuwa unapotea. Sababu ya kuanzishwa kwa bodi, maana yake tunasomesha vijana baadae wanafanya marejesho, wanapofanya marejesho tunapata nguvu ya serikali kuwasomesha vijana wengine katika kipindi cha baadae. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, kama tuna uwezo mambo yetu mazuri Wizara ya Fedha basi bado tusukume msukumo wa kuongeza mapato kwenye Bodi ya Mikopo ili baadae wanaosomeshwa waweze kufanya marejesho kuliko kupeleka pesa katika mawizara pasipo na kufanya marejesho.

Lakini pia unapopeleka mawizarani unaongeza uwezo zaidi kwa watu ambao tayari wana uwezo wa kujisomesha, kwa sababu mfanyakazi anapata fedha, lakini kijana ambaye hajaajiriwa hana njia za kupata pesa kwenda kusoma elimu ya juu. Sasa hili Mhe. Waziri, ninakuomba tuliangalie kwa kina kwamba kuna suala hilo na bodi tunajitahidi kutoa mikopo kwa ufanisi kabisa.

La mwisho, kwa vile dakika 5 amalizie Mhe. Hussein, mimi nataka nimuombe Mhe. Waziri kwamba kabla sijamalizia hilo nilikuwa na *document* hapa Mhe. Waziri wa Fedha ya Taasisi yako ya *ZRB*, katika pale niliposema kwamba watendaji wako hawako makini na wanapelekea kuikosesha pesa serikali hii

katika makusanyo, hii itakuja kukuonesha wewe uone udhaifu wa ukusanyaji wa kodi katika taasisi yako.

Namalizia kuna fununu katika kitengo cha *ZRB*, kuna mfanyakazi ameingiziwa fedha sio chini milioni 400, nataka uje unieleze Mhe. Waziri, hili lina ukweli ama halina ukweli na kama lina ukweli basi utueleze sababu za kuingiziwa fedha mfanyakazi huyu na mfanyabiashara. Kutokana na hofu hii kama kutakuwa kuna ukweli nakuomba wewe na ninaiomba serikali kupitia Kitengo cha Rushwa kuchunguza *accounts* za wafanyakazi wa *ZRB* za ndani na nje ya nchi hii. *(Makofi)*

Narudia tena Mhe. Mwenyekiti, hili kama litakuwa lina ukweli nakiomba Kitengo cha Rushwa kupitia serikali hii kuchunguza *accounts* za wafanyakazi wa kitengo cha *ZRB* za ndani na nje ya nchi, hata na zile za watu wao wa karibu kwa sababu mara nyingi wanakwepa kuingiziwa fedha katika *accounts* zenye majina yao.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru, nimesema kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Kwahani, ninaunga mkono hoja, sina matatizo, isipokuwa nataka maelezo madogo madogo Mhe. Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho. Nakushukuru sana. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Salum Haji, kwa mchango wako, lakini kabla ya kuhairisha kikao nami nichukuwe fursa ya kuwapongeza wachangiaji wote waliochangia hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango, lakini kwa wale ambao hawakupata fursa ya kuchangia hivi sasa, ninawaomba sana wapeleke michango yao kwa Mhe. Waziri, kwa maandishi na chengine kuna tangazo kidogo.

Waheshimiwa Wajumbe, bado watu wa Bima ya Afya na kesho watakuwepo mpaka Jumanne, kwa wale ambao bado hawajajaza fomu waendelee kupeleka fomu zao na kujaza fomu hizo. Kuna wachangiaji mawaziri ambao jumla yao ni 3, kwa hivyo, Jumatatu tukijaaliwa wataanza mawaziri kuchangia na baadae atafata Mhe. Waziri wa Fedha katika majumuisho yake.

Waheshimiwa Wajumbe, kesho saa tatu kutakuwa na semina tukijaaliwa, kwa hivyo, wajumbe wote mnatakiwa muwepo na semina hii inatokea katika Kitengo cha Kitaifa Kuratibu Mfuko wa Fedha wa Dunia. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, saa 3.00 mnaombwa muhudhurie.

Waheshimiwa Wajumbe, kikao nimekiahirisha mpaka siku ya Jumatatu tarehe 27/06/2016 saa 3.00 kamili asubuhi.

(Saa 6.00 Mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 27 saa 3.00 asubuhi)